Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Uelekeo

## Mafuriko yaua 341 Chad



Uk. 19

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00082 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Septemba 11 - 17, 2024 |

# Maeneo 10 ya kipaumbele cha ziara ya Samia nchini China



### MAUAJI KADA WA CHADEMA:

## Mabalozi waunga mkono agizo la Rais kusakwa waliohusika

**Na Mwandishi Wetu**

AGIZO la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan la kutaka ufanyike haraka uchunguzi wa mauaji ya kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Ally Mohamed Kibao kuwabaini wahusika ili wachukuliwe hatua za kisheria, umeungwa mkono... Uk. 4.



## Samia asikitishwa kifo cha Askofu Sendoro

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema amepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Askofu Chediel Elinaza Sendoro wa Kanisa la Kiinjili ya Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mwanga. Uk.2

## TOFAUTI TANO KATI YA MPOX NA UVIKO - 19



Uk. 7&8

# Samia asikitishwa kifo cha Askofu Sendoro

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amesema amepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Askofu Chediel Elinaza Sendoro wa Kanisa la Kiinjili ya Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mwanga.

Askofu Sendoro alifariki dunia baada ya gari alilokuwa akiendesha kugongana uso kwa uso na lori katika eneo la Kisangiro wilayani Mwanga, Septemba 9, mwaka huu, usiku.

Rais Samia alitoa pole kwa Mkuu wa KKKT Baba Askofu Dk. Alex Malasusa, Maaskofu wote, waumini, familia, ndugu, jamaa na marafiki.

"Nawaombea faraja kwa neno kutoka Biblia Takatifu kitabu cha Waebrania 13:14; 'Maana hapa hatuna mji udumuo, bali twautafuta ule ujao."

Alimuombea kwa Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya marehemu Askofu Sendoro.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

# TPA, WMA simamieni flow meter kikamilifu-Waziri Jafo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara Dk. Selemani Jafo, ameitaka Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Wakala wa Vipimo (WMA), kusimamia kikamilifu kituo cha kushushia mafuta (flow meter) kinachopima kiwango cha mafuta yanayoingia nchini ili serikali ipate mapato halisi.

Alitoa agizo hilo jana wakati akikagua kituo hicho Kurasini Oil Jet (KOJ) kilichopo Bandari ya Dar es Salaam kinachosimamiwa WMA.

Alisema Bandari ya Dar es Salaam ndiyo lango kuu la kibiashara nchini na WMA wana jukumu la kujua kiwango cha mafuta kinachoingia ili kuhakikisha serikali inapata pato halisi kutokana na mafuta hayo.

Aidha, aliipongeza Serikali kwa uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam ambao alisema umeanza kuleta tija kubwa hususan ufungaji wa mitambo ya kisasa ya flow meter inayotumika kupima kiwango cha mafuta yanayoingia nchini na kutatua changamoto iliyokuwepo muda mrefu katika upimaji wa nishati hiyo.

Pia aliipongeza TPA kwa kazi kubwa ya kuboresha upakuaji na uondoaji wa mizigo katika bandari hiyo, hali inayorahisisha biashara nchini kwa kupunguza siku za upakuaji mizigo inayoingia nchini.

Naye Kaimu MKurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abeid Garus, aliishukuru Serikali kwa uwekezaji na vifaa ambavyo vimeongeza ufanisi ambapo alibainisha kuwa awali meli ilikuwa ikitumia siku saba kupakua mzigo, lakini kwa sasa inatumia siku tatu hadi nne.

Alisema idadi ya siku za meli kusubiri kuingia bandarini awali ilikuwa hadi siku 30, lakini kwa sasa zinasubiri siku tano hadi saba hali ambayo inachagiza uboreshaji wa utoaji huduma na utendaji.

Naye Afisa Vipimo Mwandamizi wa WMA katika bandari hiyo, Tegemeo Cosmas, alibainisha kuwa kwa sasa flow meter zinahakikiwa kila mwaka na zinapima mafuta kwa usahihi mkubwa.



## Dimwa ataja mambo matano ya kujivunia

**Na Is-Haka Omar, Zanzibar**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa, ameyataja mambo matano ya kujivunia na kuungwa mkono katika uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Mwinyi tangu aingie madarakani.

Aliyataja mambo hayo kuwa ni Zanzibar yenye neema kwa wote, Zanzibar salama na yenye maendeleo endelevu.

Mengine ni Zanzibar yenye kuheshimu, kulinda na kuenzi misingi ya demokrasia na siasa za maendeleo pamoja na , Zanzibar yenye kuenzi na kulinda historia yake hasa ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Alisema hayo wakati akiwahutubia wanachama wa CCM na wananchi kwa ujumla wa Wilaya ya Micheweni katika mwendelezo wa ziara ya Wajumbe wa Sekretarieti ya Kamati Maalum ya NEC CCM Taifa, Zanzibar.

Alisema dhamira ya CCM ni kusimamia na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi unaotekelezwa na SMZ ili wananchi wa makundi yote wanufaike na fursa ya maendeleo endelevu.

Alisema Zanzibar inapiga hatua kubwa ya maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Dimwa alifafanua kuwa siri ya mafanikio hayo ni uwazi na uhuru uliowekwa na serikali kwa kufungua milango ya uwekezaji sambamba na kuweka sera na sheria rafiki katika uendeshaji wa biashara huria kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.



**Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa**



# INEC yaongeza vifaa vya uandikishaji Musoma

**Na Mwandishi Wetu, Mara**

BAADHI ya wapigakura walioshiriki zoezi la kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura mkoani Mara, wamepongeza hatua ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kuongeza vifaa vya uandikishaji katika vituo vyenye idadi kubwa ya watu.

Akizungumza baada ya kujiandikisha katika kituo cha Shule ya Msingi Songambele kilichoko Kata ya Kwamlimi Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, mmoja wa wapigakura hao, Raphael Samwel, alisema kasi ya uandikishaji wapigakura katika kituo hicho, imekuwa kubwa baada ya Tume kuongeza mashine nyingine ya uandikishaji.

Aliwataka wananchi walio na sifa ya kujiandikisha wanaokusudia kuboresha taarifa zao, kufika katika kituo hicho kwani kuongezwa kwa mashine hizo (BVR Kits), kumefanya zoezi hilo kwenda kasi na hivyo kupunguza idadi kubwa ya waliojitokeza kujiandikisha hapo.

Naye Julius Simon Rwanga aliyejiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kupitia kituo cha Shule ya Msingi Kwangwa A kilichoko Kata ya Kwanga Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, alisema wananchi wamehamasika na kujitokeza kwa wingi kushiriki kurekebisha taarifa zao, na kuishukuru Tume kwa kuongeza BVR Kits katika kituo hicho.

"Kazi ya uandikishaji leo inaenda vizuri na nina imani wote watapata fursa ya kujiandikisha tofauti na siku za nyuma," alisema.

Kwa mujibu wa Afisa Uchaguzi Manispaa ya Musoma, Deus Nyakriga, mbali na vituo vya Shule za Msingi Songambele na Kwanga A, pia Tume imeongeza BVR kits katika vituo vya Shule ya Sekondari ya Nyabisare na Chuo cha Maendeleo cha Bweri.

Alisema vituo hivyo vimeongezewa vifaa baada ya kuonekana kuwa na idadi kubwa ya wananchi hasa vijana, kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Uboreshaji wa Daftari katika mikoa ya Mara, Simiyu na baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Manyara, ulitarajiwa kukamilika jana baada ya zoezi hilo kuendeshwa katika mikoa hiyo kwa siku saba mfululizo.

# Kero ya maji Kitula kumalizika miezi minne ijayo

**Na Mwandishi Wetu, Mbinga**

KERO ya kuamka usiku wa manane na kutembea umbali mrefu kila siku kwenda kutafuta maji na kuacha shughuli za kujipatia kipato, iliyokuwa ikiwakabili wakazi wa Kata ya Kitula, Halmashauri ya Wilaya Mbinga mkoani Ruvuma, inatarajiwa kumalizika ndani ya miezi minne.

Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (Ruwasa) wilayani Mbinga, umeanza kutekeleza mradi wa maji ya bomba wa Kitula katika Kata ya Kitula, Halmashauri ya Wilaya Mbinga utakaowaondolea wananchi hiyo.

Meneja wa Ruwasa wilayani Mbinga Mashaka Sinkala, alisema mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.7 na utawanufaisha wananchi 9,100 wa vijiji vinne vya Mzuzu, Kitula, Mahilo na Lisau na kwamba utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 85.

Alitaja kazi zinazofanyika katika mradi huo kuwa ni ujenzi wa matenki matatu moja la lita 150,000 la pili la ujazo wa lita 100,000 la tatu lina uwezo wa kuhifadhi lita 75,000 na kulaza mabomba urefu wa kilometa 54.

Alisema kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa matangi yote matatu na kujenga chanzo cha maji na maji yameanza kufika kwenye matenki mawili kati ya matenki matatu kutoka kwenye chanzo.

Alisema wanasubiri mabomba ambayo yatalazwa urefu wa kilomita 10 ili kukamilisha ujenzi wa mradi huo utanaotarajia kukamilika katika kipindi cha miezi minne ijayo.

Diwani wa kata hiyo, Alex Ngui alisema mradi huo utawasaidia wananchi hao kupata huduma ya maji safi na salama kwenye maeneo yao na hivyo kupata muda mwingi wa kushiriki kazi mbalimbali za maendeleo.

# Maeneo 10 ya kipaumbele cha ziara ya Dk. Samia nchini China

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, amesema mkutano wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya Afrika na China uliofanyika nchini China hivi karibuni, una faida kubwa kwa Tanzania.

Profesa Mkumbo amesema yapo maeneo 10 yaliyopatiwa kipaumbele na Serikali ya China kupitia Rais wake, Xi Jinping.

Aliyasema hayo katika taarifa yake maalum aliyoitoa mwishoni mwa wiki.

Alieleza kuwa maeneo hayo yamelenga kuleta maendeleo nchini Tanzania yakihusisha sekta za elimu, viwanda, uwekezaji, miundombinu, na biashara.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na Rais wa China, Xi Jinping




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo

"Maeneo haya yapo ndani ya ajenda ya kuleta maendeleo Tanzania kupitia nyanja zote. Rais wa China ametangaza kufungulia soko la biashara la China kwa ajili ya bidhaa kutoka Tanzania na hakuna bidhaa itakayotozwa ushuru. Hii ni fursa kubwa na haijawahi kutokea duniani," alisema Profesa Mkumbo.

Aidha, aliongeza kuwa soko la China ni kubwa kwa bidhaa za Afrika, ikiwemo Tanzania na kwamba serikali itaendelea kuhamasisha wafanyabiashara wa Kitanzania kuchangamkia nafasi hiyo.

"Fursa hii ni ya kipekee kwa Watanzania, hasa kwa kuzingatia ukubwa wa soko la China," aliongeza.

Pia Profesa Mkumbo alizungumzia msaada wa kifedha ambao Tanzania itanufaika kupitia Dola za Kimarekani bilioni 50 (sawa na Sh. trilioni 135) zilizotengwa ambazo.

Fedha hizo zimegawanywa katika makundi matatu ambapo Dola bilioni 29 zitapokelewa kama mikopo, Dola milioni 11 zitakuwa kwa njia ya msaada na Dola bilioni 10 zitatumika kwa uwekezaji wa kampuni za China nchini Tanzania.

"Fedha hizi ni nyingi sana. Tayari nimeagiza Tume ya Mipango ifanyie kazi haraka mpango huu, kwa kuwa ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi," alisema Profesa Mkumbo na kufafanua kuwa Tanzania sipochukua hatua za haraka, fursa hiyo itapotea na fedha hizo zitapelekwa sehemu nyingine.

Aidha, amekiagiza Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kuhakikisha angalau theluthi moja ya Dola bilioni 10 zinatumiwa na kampuni za China kuwekeza nchini.

Alifafanua kuwa tayari hatua zimeanza na Rais Dk. Samia anakutana na baadhi ya wawekezaji wakubwa kutoka China ili kufanikisha malengo hayo.

"Rais amekutana na wawekezaji wakubwa na tunaamini hii ni fursa kubwa kwa Tanzania," alisema Profesa Mkumbo.

Akizungumzia ushirikiano wa Tanzania na China, Profesa Mkumbo alibainisha kuwa kila eneo la maendeleo nchini, limeguswa na Serikali ya China na sasa ni wakati wa Watanzania kuchangamkia fursa zilizopo.

"Kushindwa kutumia fursa hizi, itakuwa hasara kubwa kwa nchi yetu huku mataifa mengine yakiendelea kufaidika," aliongeza.

Pia alionya kuwa endapo Watanzania watashindwa kutumia fursa hiyo, mataifa 53 ya Afrika, yatapata faida kubwa na Tanzania itabaki nyuma.

## MAUAJI KADA WA CHADEMA:

# Mabalozi waunga mkono agizo la Rais

## ● Ni la kusakwa waliofanya kitendo hicho

**Na Mwandishi Wetu**

AGIZO la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan la kutaka ufanyike haraka uchunguzi wa mauaji ya kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Ally Mohamed Kibao kuwabaini wahusika ili wachukuliwe hatua za kisheria, umefungwa mkono na Mabalozi wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini na Canada.

Katika tamko lao la pamoja jana walisema wamesikitishwa na matukio ya hivi karibuni ya vitendo vya ukatili, kupotea kwa watu na vifo vya wanaharakati wa kisiasa na haki za binadamu nchini.

Walitoa wito wa kufanyika kwa uchunguzi wa kina kuhusu matukio hayo na kutoa pole kwa familia zote zilizoathirika.

Walisema mpango wa 4R wa Rais Dk. Samia pamoja na mambo mengine, unalenga kuhakikisha haki za msingi za wananchi na uhuru wa kujieleza unalindwa nchini.

Walitoa wito kwa Serikali kuhakikisha usalama wa raia na upinzani, wakisihi utekelezaji wa mpango wa Rais Dk. Samia Suluhu wa 4R.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, amesema wakati umefika kwa wote wenye madaraka Kikatiba na kisheria ya kuhudumia Watanzania kwa mahitaji yao yote, wawajibike.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kufuatia taarifa za kutekwa, kuteswa, kupotezwa na wengine kuuawa.

Katika tukio la hivi karibuni la mauaji ya kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Ali Mohamed Kibao, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameviagiza vyombo vya ulinzi kuchunguza mauaji hayo na kumpelekea ripoti haraka.

> "Mpango wa 4R wa Rais Dk. Samia pamoja na mambo mengine, unalenga kuhakikisha haki za msingi za wananchi na uhuru wa kujieleza unalindwa nchini.

# Askofu David Mwasota amlilia Askofu Dk. Chedieli Sendoro




Askofu David Mwasota

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Naioth Gospel Assembly (NGA), Mchungaji Dk. David Mwasota, ametoa salamu za pole kwa Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Alex Malasusa kwa msiba wa Mchungaji Dk. Chedieli Elinaza Sendoro (CPA, PhD), aliyekuwa Askofu wa KKKT Dayosisi ya Mwanga.

Mchungaji Dk. Sendoro, alifariki dunia kwa ajali ya gari Septemban 9, mwaka huu.


Katika salamu hizo za pole kwa niaba ya Kanisa la Naioth alizozitoa Makao Makuu ya kanisa hilo yaliyopo eneo la External Makuburi jijini Dar es Salaam, Askofu Mwasota ambaye pia ni Katibu Mkuu Mstaafu wa Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), alimwelezea marehemu Askofu Sendoro kama mtumishi aliyekuwa `future' njema kwa KKKT, jamii ya Kikristo na Watanzania kwa ujumla.

Askofu Mwasota alisema sasa ni jukumu la wote kumwombea faraja Mkuu wa KKKT na Kanisa kwa ujumla Dk. Malasusa kwa kupoteza kiongozi,Lakini pia kuwaombea faraja ya Kristo familia ya marehemu Askofu Sendoro na wafiwa wote kwa ujumla.

Askofu Sendoro wa KKKT Dayosisi ya Mwanga, alifariki dunia Septemba 9, mwaka huu baada ya gari alilokuwa akiliendesha kugongana uso kwa uso na lori eneo la Kisangiro, Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro.

Wakati huo huo, Padri Nicolaus Ngowi wa Shirika la Damu Azizi ya Yesu, amefariki dunia katika ajali ya gari iliyotokea jana alasiri mkoani Kilimanjaro.

Taarifa rasmi ya kifo chake imetolewa na Mkuu wa Shirika Provision ya Tanzania, Padre Vedasto Ngowi.




Askofu Dk. Chedieli Elinaza Sendoro

# Mhadhiri atoa ushauri mzito kwa wazazi maadili ya watoto

**Na Gustaphu Haule**

WAZAZI wametakiwa kushirikiana na walimu katika suala la kudhibiti maadili ya watoto. Wito huo ulitolewa na Mhadhiri wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Frida Ilomo alipokuwa akizungumza na walimu, wazazi na wanafunzi katika mahafali ya darasa la saba ya Shule ya Msingi Mount Calvary iliyopo Kiluvya kwa Komba, Kata ya Kibamba, Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Ilomo alisema suala la kudhibiti vitendo vya mmomonyoko wa maadili kwa wanafunzi, linahitaji ushirikiano kati ya walimu na wazazi.

Alisema wazazi wanapaswa kusimamia mienendo ya watoto wao kila uchao ikiwa ni pamoja



na kuwaeleza masuala mazuri ya kuwajenga katika maadili mema kuliko kuwaachia walimu wafanye kila kitu.

Mhadhiri huyo alisema wazazi wengi hufanya makosa makubwa ya kujisahau juu ya malezi ya watoto wao kwani wakishamkabidhi mtoto kwa walimu wao, hujiona wamehitimisha kazi na kubaki kuendelea na mambo mengine bila kutaka kujua maendeleo ya mtoto wake akiwa shuleni.

Alisema kitendo hicho ni kibaya kwani jukumu la kulea mtoto linapaswa kuwa shirikishi baina ya walimu, mzazi na hata jamii na hivyo kuwataka wazazi kuanza kubadilika kwa ajili ya kuhakikisha watoto wao wanawajengea misingi imara.

Akitolea mfano wanafunzi waliomaliza darasa la saba katika Shule ya Msingi Mount Calvary, Ilomo alisema kuwa shule hiyo inawafundisha katika misingi ya kidini na humaliza wakiwa na maadili mema, lakini jukumu lililobaki ni kuhakikisha wazazi wanayalinda maadili hayo.


"Niwaombe sana wazazi, wahakikishe maadili waliyofundishwa wanafunzi hawa hapa shuleni wakayaendeleze maana wakiacha, wanaweza kuingia katika makundi mabaya yasiyo na afya kwao" alisema Ilomo.

Na katika hatua nyingine, Ilomo ameahidi kusaidia kutatua baadhi ya changamoto zilizopo katika shule hiyo ikiwemo ujenzi wa bwalo, kusaidia katika ununuzi wa kompyuta za kufundishia pamoja na mahitaji mengine.

Akisoma risala mbele ya mgeni rasmi, mwanafunzi anayemaliza darasa la saba shuleni hapo, Anthony Juvent, alisema shule hiyo imewajenga kimaisha na kimasomo kutokana na kufundisha kiimani.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

HII NI KERO




## Kupiga na kusikiliza simu kwenye vivuko vya zebra

BAADHI ya watu wamekuwa na tabia ya kutumia simu zimu zao kwa kupiga, kuzungumza, kupokea ama hata kuchat kwa simu zao wakati wakivuka kwenye alama za pundamilia (zebra) bila kujali usalama wao, wa wenzao na vyombo vya moto.

Hii ni kero kwa madereva wa magari na vyombo vingine vya moto kwani eneo hilo linapaswa kutumika na waenda kwa miguu kwa uangalifu ili kuepusha ajali.

Ni busara kuacha matumizi ya namna hiyo hata kama simu itaita ukiwa unavuka eneo hilo, usipokee badala yake subiri mpaka umalize kuvuka na kuwa katika eneo salama.




MAONI YA MHARIRI

## Tunaunga mkono agizo la Rais mauaji ya kada wa Chadema

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ameviagiza vyombo vya uchunguzi kufanya uchunguzi wa haraka kufuatia kifo cha aliyekuwa Msaidizi Maalum wa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Ally Mohamed Kibao.

Kadhalika, Rais Dk. Samia ameviagiza vyombo hivyo kufanya uchunguzi wa namna hiyo kwa matukio mengine yanayoshabihiana na hilo. Agizo hilo limeungwa mkono kwa kauli moja na Mabalozi wa Nchi za Jumuiya ya Ulaya (EU) na Canada wa hapa nchini.

Katika tamko lao la pamoja jana, Mabalozi hao walisema wamesikitishwa na matukio ya hivi karibuni ya vitendo vya ukatili, kupotea kwa watu na vifo vya wanaharakati wa kisiasa na haki za binadamu nchini na kutoa wito wa kufanyika kwa uchunguzi wa kina kuhusu matukio hayo, lakini pia wakatoa pole kwa familia zote zilizoathirika.

Rais Dk. Samia, alitoa agizo hilo siku moja tu baada ya tukio hilo la kuuawa kwa kada huyo wa Chadema.

Hii inadhihirisha kuwa, Rais Dk. Samia anaheshimu na kutekeleza kwa vitendo utawala wa sheria kutokana na ukweli kwamba ameviagiza vyombo vya uchunguzi vifanye uchunguzi wa haraka kuwabaini watu waliofanya kitendo hicho ili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria za nchi.

Sisi tunaamini kwamba Rais Dk. Samia ana nia ya dhati ya kutaka wauaji na wote wanaofanya vitendo vya kikatili dhidi ya binadamu wenzao, wanawajibika kwa mujibu wa sheria.

Tunaunga mkono kwa msimamo huu ambao unaonyesha jinsi Kiogozi wa Nchi anavyojali maisha ya Watanzania. Tungependa vyombo husika vilivyoagizwa, kutekeleza agizo la Rais Dk. Samia kwa wakati, lakini pasipo kumuonea mtu yeyote.

Ieleweke wazi kwamba mpango wa 4R wa Rais Dk. Samia pamoja na mambo mengine, unalenga kuhakikisha haki za msingi za wananchi na uhuru wa kujieleza unalindwa.

Aidha, tunawaomba na kuwashauri wananchi kutulia wakati huu vyombo vya uchunguzi vikiendelea kutekeleza agizo hilo na tunaamini kwamba wale wote watakaobainika kuhusika na tukio hilo na mengine ya namna hiyo, sheria itachukua mkondo wake.


## Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255784122020 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |




Hamid Yassin
JICHO LANGU
0768 888 787

## Tuwe macho na wanaokerwa na urafiki wetu na China

RAIS Samia alikuwa nchini China kwa ziara ya siku tano kuanzia Septemba 2 hadi 6 ambapo pamoja na mambo mengine, pia alihudhuria Mkutano wa Nne wa Ushirikiano wa China-Afrika (FOCAC).

Baada ya mkutano ule wa mwaka huu, pia alifanya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais Xi Jinping, ya kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo.

Malengo makubwa kwenye ziara hiyo yalikuwa ni kwenye uchumi, uhusiano kati ya watu, maendeleo, teknolojia masuala ya kimataifa, usalama na nishati safi.

Naam; tangu jukwaa hili lilipoanzishwa mwaka 2000, huu ulikuwa mkutano wa tisa wa FOCAC, na kila upande, una matarajio makubwa kwa jukwaa hili, kwa sababu limekutanisha tena wakuu wa nchi na serikali kutoka Afrika na China, wanakutana na Rais Xi Jinping hapa, ambapo pamoja na mambo mengine, wamejadili ushirikiano kati ya Bara la Afrika na China.

Uhusiano huu wa kidiplomasia kati ya Tanzania na China umekuwapo tangu 1964, ikiwa ni miongo sita sasa ambao ulianza kwa kuwa na aina moja ya idiolojia sawa, imani sawa kuhakikisha uhuru wa nchi zote, mamlaka na umoja wa eneo, kujitolea kwetu dhidi ya ukoloni na ushirikiano.

Uhusiano huu ulizidi kukua hadi kuwa uhusiano wa chama kwa chama, ushirikiano wa kiuchumi, uhusiano kati ya watu, na nyanja nyingine muhimu pia.

Ikumbukwe mwaka 2022 marais wa Tanzania na China walikubaliana kuimarisha uhusiano huo na kuwa wa kina zaidi kwa manufaa ya pande zote.

Kuna maeneo muhimu matatu au manne; moja ni kuhusu maendeleo ya miundombinu, wakati mwingine tunapozungumzia China na Tanzania, jambo la kwanza linalokuja akilini mwa wengi ni reli ya Tazara.

Hii ilikuwa mwanzo wa ushirikiano mkubwa wa miundombinu. Na tunavyofahamu, miundombinu ni muhimu sana kwa kufungua uchumi wa nchi yoyote, kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko, kuunganisha nchi na sehemu nyingine za dunia.

> **China imekuwa mshirika wetu mkuu wa kibiashara, kwa miaka minane au tisa iliyopita. China ndiyo nambari moja kama mshirika wa kibiashara na tunavyofahamu.**


Tuelewe kuwa, siyo miundombinu tu, kuna eneo la pili la upande wa uzalishaji, China tangu wakati wa miaka ya 1960 hadi sasa, imekuwa ikisaidia Tanzania katika maeneo ya uzalishaji, kilimo, utengenezaji.

China imekuwa mshirika wetu mkuu wa kibiashara, kwa miaka minane au tisa iliyopita. China ndiyo nambari moja kama mshirika wa kibiashara na tunavyofahamu, biashara ni muhimu sana kwa ustawi, bila kusahau sekta ya utalii.

Kutokana na ukweli kwamba Bara la Afrika lina raslimali nyingi, limekuwa likimezewa sana mate na mataifa makubwa. Kwa maana hiyo hayafurahishwi sana na uswahiba wa Afrika na mshirika huyu ambaye hana kawaida ya kuingilia masuala ya ndani ya nchi zetu na kutoa masharti magumu magumu.

Kamwe tusikubali matifa ya magharibi yatufarakanishe na China kwa faida zao za kibiashara! Tushimane na Rais wetu Dk. Samia katika kuustawisha uhusiano huu ili uwe jadidi!

# Tofauti tano kati ya Mpox na Uviko - 19



**Tunajua jinsi ya kudhibiti mpox. Katika kanda ya Ulaya, tunajua hatua zinazohitajika ili kuondoa maambukizi yote. Magonjwa yote mawili, husababishwa na virusi, lakini yana dalili tofauti na huenea kwa njia tofauti.**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) lilipotangaza mpox kuwa dharura ya kiafya ya kimataifa kwa mara ya pili katika kipindi cha miaka miwili, baadhi ya watu waliuliza: Je, hii ndiyo Covid-19 mpya?

Hata hivyo, wanasayansi wanasema, `hapana.'

"Mpox siyo Covid mpya. Hatari ya mpox kwa watu, ni ndogo," anasema Dk. Hans Kluge, mkurugenzi wa kanda wa WHO barani Ulaya.

"Tunajua jinsi ya kudhibiti mpox. Katika kanda ya Ulaya, tunajua hatua zinazohitajika ili kuondoa maambukizi yote.

Magonjwa yote mawili, husababishwa na virusi, lakini yana dalili tofauti na huenea kwa njia tofauti.

"Kuna tofauti nyingi zaidi kuliko kufanana," anasema Profesa Rodney Adam, Mtaalamu wa Magonjwa ya Kuambukiza katika Hospitali ya Chuo Kikuu cha Aga Khan nchini Kenya.

**MPOX SIYO VIRUSI VIPYA**

Mpox, ambayo hapo awali ilijulikana kama monkeypox, imekuwepo tangu mwaka 1958 na virusi hivi viligunduliwa kwa mara ya kwanza kwa nyani waliofungiwa nchini Denmark.

Kisa cha kwanza kwa binadamu kiliripotiwa katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC) mwaka 1970.

Tangu wakati huo kumekuwa na milipuko Afrika Magharibi na Kati.



Mara ya kwanza kutangazwa kuwa dharura ya kiafya duniani, ilikuwa ni mwaka 2022, ugonjwa huo ulikuwa umeenea katika nchi zaidi ya 70.

Lakini mlipuko wa mwaka 2019 wa Uviko-19 huko Wuhan, China, ambao ghafla ukawa janga la ulimwengu, ulitokana na virusi vipya vya SARS-CoV2 - ambavyo havijatambuliwa hapo awali kwa wanadamu.

Wanasayansi wanasema wanajua zaidi kuhusu mpox kuliko wanavyojua kuhusu Uviko-19 ilipokuwa dharura ya afya kwa dunia.

Ingawa magonjwa yote mawili huenezwa kwa njia ya mawasiliano ya kimwili, Uviko-19 huenea haraka kwa njia ya hewa.

Watu wanaweza kuupata kwa kuvuta matone madogo ya majimaji kutoka kwa mtu aliyeambukizwa ambaye anakohoa, kupiga chafya, kuzungumza, kuimba au kupumua mbele yako, kwa

Inaendelea uk. 8

# Tofauti tano kati ya Mpox na Uviko - 19

Inatoka uk. 7

mujibu wa WHO.

Mpox huenezwa kwa kugusana kwa karibu sana au kwa muda mrefu na mtu aliyeambukizwa, kama vile kugusana ngozi kwa ngozi, ikiwa ni pamoja na wakati wa ngono na kugusa matandiko na nguo zenye maambukizi.

Zaidi ya kesi milioni 760 za Covid-19, zilirekodiwa ulimwenguni kati ya Desemba, mwaka 2019 na Agosti, mwaka 2023, WHO inasema, imechukua miaka miwili tangu Mei, mwaka 2022 kwa maambukizi ya mpox kufikia watu 100,000 ulimwenguni.

Mwaka huu, Kituo cha Afrika cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (Africa CDC), kimerekodi kesi 18,910 na karibu vifo 600.




#### CHANJO ZIPO TAYARI KWA MPOX

Mwanzoni mwa janga la Covid-19, kulikuwa na mbio za kutengeneza chanjo. Lakini chanjo zinazotoa kinga dhidi ya mpox zinapatikana sasa.

Mpox inahusiana na ugonjwa wa ndui, ugonjwa ambao ulimwengu uliutokomeza kupitia chanjo mwaka 1980.

Chanjo zilizofanya kazi dhidi ya ndui pia zinatoa kinga dhidi ya mpox, hasa katika mlipuko wa mwaka 2022.

"Siyo kinga kwa asilimia 100, lakini kulingana na mlipuko mkubwa wa mwaka 2022 huko Ulaya na Amerika Kaskazini, wazee walikuwa katika hatari ndogo na hiyo inadhaniwa kuwa ni kwa sababu walikuwa na kinga kutoka chanjo ya ndui," anasema Profesa Adam.

Bavarian Nordic ilitoa zaidi ya dozi milioni 15 za chanjo ya MVA-BN - chanjo ya mpox inayotokana na chanjo ya ndui kwa zaidi ya nchi 76 duniani kote wakati wa mlipuko wa mwaka 2022.

#### VIRUSI VYA MPOX HUBADILIKA POLEPOLE

Baadhi ya Virusi hubadilika haraka kuliko vingine. Ni kwa sababu mpox husababishwa na virusi vya DNA na Covid-19 husababishwa na virusi vya RNA.

Virusi vya DNA havibadiliki kwa uhuru kama virusi vya RNA kulingana na wataalamu.

Kuna familia mbili zinazojulikana au makundi ya virusi vya mpox - clade 1 na clade 2.

Virusi vya SARS-CoV2 vina zaidi ya makundi 20 yanayojulikana.

Mlipuko wa sasa unasababishwa zaidi na virusi vya clade 1, vinayojulikana kama clade 1b.

Wanasayansi wa WHO wanasema hawajui kama aina ya 1b inasambazwa kwa urahisi zaidi kuliko aina nyinginezo.

Wanachojua ni kwamba katika mlipuko wa hivi sasa, watu walioambukizwa huwa tayari wamepata dalili kali wanaripoti kuwa na ugonjwa huo.

#### HAKUNA UWEZEKANO WA KARANTINI

Watu wengi wana wasiwasi kwamba kuenea kwa mpox kutasababisha shughuli kufungwa, kama tulivyoona katika janga la Covid.

Ingawa ugonjwa huo umeenea katika mataifa 16 barani Afrika kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita, CDC Afrika haipendekezi kufungwa kwa mipaka.

"Afrika CDC, kwa wakati huu na ushahidi tulionao, haishauri kukatizwa kwa safari za watu na bidhaa," anasema Dk Jean Kaseya, Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo.

"Safari za watu na bidhaa zitaendelea kama ilivyokuwa zamani, wakati tunapambana na janga hili."

Dk. Mike Ryan, Mkurugenzi Mtendaji wa Mpango wa Dharura wa Afya wa WHO, anakubali.

"Mpox ni virusi ambavyo vinaweza kudhibitiwa ikiwa tutafanya mambo kwa njia sahihi kwa wakati unaofaa na kuweka akili zetu zote katika mapambano.

#### KAMA TULIVYOFANYA KWA COVID.

Mpox kawaida huwa haina nguvu na watu wengi hupona ndani ya wiki mbili hadi nne. Lakini, watu wengine hupata ugonjwa mbaya na huhitaji kulazwa hospitalini.

Unaweza kujikinga na maambukizi kwa kuepuka kuwasiliana kwa karibu na watu walioambukizwa, vitu au wanyama. Unawaji mikono au kutumia vitakatisha mwili, baada ya kugusa vidonda na majeraha.

"Tunajua kwamba chanjo ni kinga, kwa hivyo tuna zana bora zaidi kwa sasa, kwa virusi visivyoambukiza sana," anasema Profesa Rodney na kuongeza:

"Kwa hiyo, janga kama Covid nadhani haliwezekani."

BBC.



*Leo ndiyo, kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Septemba 11 - 17, 2024 |

UTALII

AFYA

JAMII

Jarida hili haliuzwi



# China ilivyoahidi makubwa

UK. 12 & 13



# Samia: China ni rafiki akujuae kwa dhiki na raha

**Na Mwandishi Wetu**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuanzia Septemba 2 hadi 6, 2024 alikuwa miongoni mwa wakuu wa nchi na serikali 53 walioshiriki kwenye Mkutano wa tisa wa Wakuu wa Baraza la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC).

Mkutano huo ulipata mwitikio mkubwa, si tu kutoka kwa wakuu wa nchi na serikali wa Afrika, bali pia viongozi na watendaji kutoka taasisi na mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa, huku ukifuatiliwa na mamilioni ya watu kote duniani.

Rais Samia alikuwa miongoni mwa viongozi wachache kutoka Afrika waliohutubia mkutano huo akiwakilisha ukanda wa Afrika Mashariki.

Marais wengine kutoka Afrika waliohutubia mkutano huo ni pamoja na Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini, Bassirou Diomaye Faye wa Senegal, Mohamed Ould Ghazouani wa Mauritania, Denis Sassou Nguesso wa Jamhuri ya Congo na Bola Ahmed Adekunle Tinubu wa Nigeria.

Katika hotuba yake, Rais Samia anaeleza kuhusu umuhimu wa ushirikiano wa kimkakati katika kuchagiza maendeleo na kutoa wito kwa pande zote mbili kuendelea kuunganisha nguvu ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili.

### CHINA NI CHACHU KATIKA KUKUZA UCHUMI AFRIKA

Rais anasema matokeo ya ushirikiano imara na madhubuti kati ya China na Afrika yanadhihirika kupitia maendeleo makubwa ambayo nchi nyingi za Afrika zimeyapata kupitia ushirikiano huo.

"Ushirikiano baina ya China na Afrika umekuwa chachu katika kukuza uchumi wa nchi nyingi za Afrika pamoja na kuleta mendeleo ya watu kupitia miundombinu na ukuaji wa maendeleo ya viwanda vidogo na vikubwa," anasema.

### CHINA NI RAFIKI WA UKWELI

Rais anasema Serikali ya China imeendelea kuwa rafiki wa kweli kutokana na utekelezaji wa makubaliano na maendeleo mbalimbali kati ya nchi za Afrika na China.

"Licha ya changamoto zilizoukabili uchumi wa dunia kwa miaka ya hivi karibuni, Serikali ya China imeendelea kuwa rafiki wa kweli kwa kuhakikisha utekelezaji wa kiwango cha juu cha makubaliano yaliyofikiwa katika mikutano mbalimbali ya Jukwaa la Ushirikiano," anasema Rais Samia na kutaja moja ya changamoto ambayo China ilikutana nayo ni Uviko 19.

Anaendelea, "China imekuwa rafiki yetu katika mapambano dhidi ya umaskini na kuleta maendeleo. Hili kunadhihirika kwenye miundombinu na ukuaji wa viwanda vidogo na vya kati katika mataifa yetu.

Rais anasema Mpango wa FOCAC wa Beijing wa 2025/27 unajibu mahitaji mengi ya Afrika.

Rais Samia anakumbusha kwamba mkutano wa Beijing umefanyika ikiwa imepita mwongo mmoja tangu Rais Xi Jinping alipotangaza mkakati wa China - Afrika jijini Dar es Salaam mwaka 2013 alipofanya ziara yake ya kwanza Barani Afrika.

Rais anasisitiza nia ya kujitolea kwa Tanzania kuimarisha ushirikiano wake na China, hasa katika miundombinu na maendeleo ya kiuchumi.

Aidha, Rais Samia anaonesha umuhimu wa ushirikiano katika sekta kama kilimo, biashara, na teknolojia rafiki wa mazingira.

Hotuba ya Samia ilijumuisha mipango ya China kuwekeza dola bilioni 50 katika Afrika kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo, kwa lengo la kuimarisha miundombinu, biashara, na kuunda ajira mpya.

Tanzania inatarajiwa kunufaika kutokana na ushirikiano huu, ambao pia utachochea ushirikiano wa kikanda na ukuaji wa kiuchumi.

Jambo moja muhimu lililozungumziwa katika mkutano huo ni kufufua mradi wa reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), ambapo China imeahidi kuunga mkono kwa kiasi kikubwa.

Makubaliano hayo, yaliyosainiwa mbele ya Rais Xi Jinping na Rais wa Zambia Hakainde Hichilema, yanalenga kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kukuza biashara za kikanda, hivyo kuimarisha nafasi ya Tanzania kama kitovu cha kikanda.

Katika hotuba yake kwenye mkutano wa tisa wa Baraza la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC), Rais Xi anasema nchi yake itashirikiana na Afrika katika mafunzo ya pamoja, biashara, uwekezaji, viwanda, ubia katika sekta ya afya na kukuza kilimo ili kuwanufaisha Waafrika.

Pia anasema China iko tayari kufadhili miradi ya kutunza mazingira na ushirikiano katika sekta ya usalama.

Rais Xi anasema katika mipango 10 ya mahusiano ya China na Africa, nchi yake ipo tayari kujitolea kwa dhati kuleta na kutafuta maendeleo yenye malengo ya kisasa yaliyoainishwa katika Ajenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika.

Anasema wakati China na Afrika zikitekeleza ndoto ya kisasa, bila shaka pande hizo mbili zitaanzisha ongezeko la maendeleo ya kisasa (modernization) duniani na kuandika sura mpya katika kujenga jumuiya ya mustakabali wa pamoja kwa wanadamu.

### UHUSIANO WA CHINA NA TANZANIA

Uhusiano wa Tanzania na China ni wa kihistoria, kiuchumi, na kidiplomasia, ulioanza tangu enzi za mapambano ya uhuru wa Afrika. Uhusiano huo umekuwa wa kirafiki na wa karibu, ukijikita katika nyanja za siasa, uchumi, na utamaduni.

### KIPINDI CHA KIHISTORIA

Uhusiano wa kidiplomasia rasmi kati ya Tanzania na China ulianza mwaka 1964, mara baada ya kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Moja ya mradi mkubwa ulioweka msingi wa ushirikiano wa nchi hizi ni Reli ya TAZARA (Tanzania-Zambia Railway), ambayo ilijengwa kwa msaada wa China miaka ya 1970.

Reli hii ilikuwa muhimu kwa sababu ililenga kusaidia usafirishaji wa bidhaa bila kutegemea bandari za kusini mwa Afrika ambazo zilikuwa zinadhibitiwa na makaburu waliokuwa wakitawala Afrika Kusini pamoja na wakoloni.

### USHIRIKIANO WA KIUCHUMI

Katika nyakati za sasa, China ni mshirika mkubwa wa kiuchumi kwa Tanzania. China inawekeza katika miradi mbalimbali ya miundombinu kama vile ujenzi wa barabara, madaraja, bandari, na viwanja vya ndege. Tanzania ni sehemu muhimu ya mpango wa "Belt and Road Initiative" wa China, ambao unalenga kuimarisha miundombinu na biashara kimataifa.

Bidhaa zinazoagizwa kutoka China hadi Tanzania ni pamoja na vifaa vya kielektroniki, mashine, na nguo, wakati Tanzania inauza mazao ya kilimo kama vile pamba, chai, na kahawa. Aidha, wawekezaji wa Kichina wanashiriki kwenye sekta za kilimo, madini, na viwanda nchini Tanzania.

### USHIRIKIANO WA KIDIPLOMASIA

China imekuwa ikiiunga mkono Tanzania katika masuala ya kimataifa, na nchi hizi mbili zinaendelea kushirikiana kwenye majukwaa mbalimbali ya kimataifa kama Umoja wa Mataifa (UN) na Jumuiya ya Afrika (AU). Mara kwa mara, viongozi wa Tanzania na China wamekuwa wakifanya ziara za pande mbili ili kuimarisha uhusiano wao.

### USHIRIKIANO WA KIELIMU NA UTAMADUNI:

Katika nyanja ya elimu, China imekuwa ikitoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Tanzania kwenda kusoma nchini China. Pia, vituo vya utamaduni kama Chuo cha Confucius vimeanzishwa Tanzania ili kukuza lugha na utamaduni wa Kichina.

Kwa ujumla, uhusiano wa Tanzania na China umeendelea kuimarika, huku ukilenga kukuza maendeleo ya kiuchumi na ushirikiano wa kidiplomasia baina ya nchi hizi mbili.

Na Dk. Reubeni Lumbagala



# Ziara ya Rais Samia China na matarajio chanya

Rais Samia Suluhu Hassan amehitimisha ziara yake ya kikazi ya siku tano nchini China aliyoianza Septemba 2 hadi 6, 2024.

Ziara hiyo ya kikazi nchini China imemwezesha Rais Dk. Samia kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (Forum on China-Africa Cooperation-FOCAC) jijini Beijing, China. Ni ziara ambayo bila shaka itawaletea neema kadhaa Watanzania.

Neema moja wapo ni ahadi ya Rais wa China, Xi Jinping kwa Afrika ikiwa ni pamoja na fedha kwa ajili ya kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo na ushirikiano katika sekta na nyanja mbalimbali.

Lakini neema nyingine ambayo sasa Watanzania wanaitegemea na kusubiri ni wafanyabiashara ambao Rais amewakaribisha kujua kuwekeza nchini kwa maana ya kuleta mitaji na ujuzi kwa Watanzania sambamba na China kufungua milango ya kupokea bidhaa za Tanzania.

Kupitia ziara hiyo Rais Samia amekutana na mwenyeji wake, Rais wa China, Xi Jinping kwa mazungumzo ya kuimarisha uhusiano mzuri wa kihistoria kati ya Tanzania na China ulioasisiwa miaka 60 iliyopita.

Tangu aingie madarakani Machi, 2021, Rais Samia amejipambanua kuwa mwanadiplomasia makini na mahiri ambaye anafanya juhudi kubwa ya kuiunganisha Tanzania na mataifa megine, na mahusiano hayo yanakuwa na tija katika kukuza uchumi (diplomasia ya uchumi).

Kwa kuwa nchi zinategemeana katika maendeleo, Tanzania hainabudi kuunda ushirikiano wenye tija na mataifa mengine kama njia mojawapo ya kukuza maendeleo ya nyanja zote za maisha ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni kwa kujifunza kwa wengine namna wanavyofanya ili kutimiza azma ya kukuza maendeleo ya nchi zao.

Mara zote Rais Dk. Samia anapofanya ziara nje ya nchi, ajenda ya kuvutia uwekezaji na kutangaza fursa tulizo nazo amekuwa akiipa kipaumbele kikubwa kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo ya nchi

Kiukweli Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Dk. Samia imekuwa rafiki wa wawekezaji wa ndani na nje, na imekuwa ikiwapa kila aina ya ushirikiano unaohitajika ili kutimiza azma ya kuwekeza nchini kwa kuhakikisha uwekezaji huo una tija hasa katika kuongeza fursa za ajira, kuongeza mapato na kuboresha huduma za kijamii kwa ujumla wake.

Katika dunia ya sasa, nchi zinashindana kibiashara na uzalishaji lakini pia zinashirikiana katika mambo mbalimbali kama biashara, kupambana na ugaidi, mabadiliko ya tabianchi na kadhalika.

Akiwa jijini Beijing, China, Rais Samia alikutana na kuzungumza na wawekezaji na viongozi wa kampuni mbalimbali za China kwa lengo la kuvutia uwekezaji nchini Tanzania.

Mathalani, Rais alizungumza na kampuni kubwa za nchini humo zikiwemo China Academy of Space Corporation (CASC), China Electronics Corporation, Transsion Group, Weihua Group, China Railway Construction Corporation (CRCC), Acme Consultant Engineers PTE Limited na CND.

Rais Samia amesisitiza juu ya mazingira mazuri ya kiuwekezaji na biashara yaliyowekwa na serikali yake katika kuharakisha maendeleo.

Aidha, Rais Samia aliwaalika Watanzania wakiwemo wafanyakazi, wanafanyabiashara na wanafunzi waishio China (Diaspora) kuja kuwekeza nchini ili nao kuwa sehemu ya maendeleo ya nchi.

Rais Samia alisisitiza kuwa zipo fursa lukuki za kiuchumi huku akiwahakikishia diaspora kuwa serikali imefanya maboresho ya sera na sheria mbalimbali ili kutoa na kuongeza fursa za kiuwekezaji nchini Tanzania.

"Nyumbani tuko vizuri. Mfano sasa hivi safari ya kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma inachukua saa 3 hadi 4 pekee kwa kutumia treni yetu mpya tuliyoizindua hivi karibuni. Tumefanya maboresho makubwa ya sera na sheria ili kuwapa fursa za kuendesha shughuli za kiuchumi kwa urahisi. Njooni muwekeze nyumbani," amesema Rais Dk. Samia.

Diaspora na wawekezaji wengine kutoka China wanayo nafasi ya kuwekeza nchini hasa katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda, uchumi wa buluu, biashara na teknolojia ili kukuza uchumi wao binafsi na wa Tanzania pia.

Aidha katika ziara hiyo Rais Samia aliunadi vyema mradi wa Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) unaosimamia kwa karibu na Wizara ya Kilimo katika kuhakikisha vijana wanashiriki kikamilifu katika kilimo ili kuchangia maendeleo.

Kwa hakika, ziara hii imekuwa na manufaa makubwa kwani ni katika ziara hii Rais Samia, Rais Jinping na Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema walishuhudia uwekaji saini wa hati ya makubaliano ya uboreshaji wa reli ya ushirikiano wa Tanzania na Zambia (TAZARA) ambao kukamilika kwake kutakuza sekta ya biashara, utalii na viwanda baina ya Tanzania na Zambia.

Itoshe kusema ziara za Rais Samia nyuma yake zimebeba ajenda za kusukuma maendeleo ya nchi yetu kwa kuhakikisha tunashirikiana na wadau wengine wa nje ya nchi kukuza maendeleo ya Tanzania, na huu ndio msingi wa diplomasia ya uchumi iliyopewa mkazo mkubwa na serikali ya Dk. Samia Suluhu Hassan.

Waziri wa Mambo ya Nje wa zamani, January Makamba alipata kusema kwamba huwezi kukaa ndani, ukajifungia bila kushirikiana na mtu nje halafu ukategemea maendeleo na badala yake hata maendeleo yako ya ndani na matarajio hayatatimia.

Alisema Tanzania tunaheshimika sana huko nje lakini kuheshimika huko kunatokana na kuwa na misimamo katika masuala ya kimataifa, kauli zetu na maendeleo yetu ya ndani.

Si siri kusema kwamba Rais Samia amerejesha uhusiano wa Tanzania na mataifa mengine yakiwemo ya Magharibi kwani tulijaribu kujufungia lakini matokeo hayakuwa mazuri sana.

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Maoni: 0620 800 462.*

# China ilivyoahidi makubwa Afrika

**■ Kutoa Dola bilioni 50 ■ Kutoingilia masuala ya ndani ya nchi ■ Kwenda pamoja na Afrika safari ya maendeleo ■ Yataja vipaumbele 10 vya ushirikiano**

**Na Hamisi Kibari**

SEPTEMBA 5, 2024, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Xi Jinping alizungumza na viongozi takribani 53 wa nchi za Afrika katika Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) jijini Beijing.

Katika hotuba yake hiyo, Rais Xi alitoa ahadi na ramani ya namna Taifa hilo linalotajwa sasa hivi kuwa la pili kwa uchumi mkubwa duniani baada ya Marekani litakavyokuwa likishirikiana na Afrika.

**DOLA BILIONI 50**

Katika ahadi hizo, China ilitangaza kutoa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 50 (zaidi ya shilingi trilioni 139) zitakazoelekezwa katika kusaidia masuala mbalimbali ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa mataifa ya barani Afrika. Hizi ni fedha nyingi sana, zaidi ya Bajeti nyingi za mwaka za nchi za Afrika.

Rais Xi anafafanua kwamba kuwa kiasi hicho cha fedha kitaelekezwa katika sekta mbalimbali kwa lengo la kuchagiza maendeleo ya pande zote mbili bila kuathiri misingi na taratibu za Taifa husika.

Anazidi kufafanua kwamba kiasi hicho cha fedha kitaelekezwa katika maeneo 10 ya kipaumbele ya ushirikiano wa kimkakati baina ya China na Afrika.

Anasema fedha hizo linalenga katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na usasa huku akisisitiza kuwa hakuna Taifa litakalo baki nyuma katika maendeleo hayo.

Rais Xi Jinping ameyataja maeneo hayo ya ushirikiano wa kimkakati kuwa ni ubia katika ushirikiano wa maendeleo (partnership action for development cooperation), Afya (partnership action for health), kilimo na ustawi (partnership action for agriculture and livelihood), mwingiliano wa watu na watu (partnership action for people to people exchanges), maendeleo ya kijani (partnership action for green development) na masuala ya ulinzi na usalama (partnership action for common security).

Maeneo mengine yaliyoainishwa ni ushirikiano katika viwanda (partnership action for industrial chain cooperation), mawasiliano (partnership action for connectivity), ubia katika kukuza biashara (partnership action for trade prosperity) na ubia katika mafunzo (Partnership Action for Mutual Learning among Civilizations).

Aidha Rais Xi anafafanua kuhusu mgawanyo wa dola za Marekani bilioni 50 zitakazotolewa kama ifuatavyo: bilioni 29 zitaelekezwa katika mikopo, bilioni 11 zitaelekezwa kwenye misaada ya aina mbalimbali na bilioni 10 zitaelekezwa katika uwekezaji kupitia kampuni za China zitakazokuja kuwekeza katika nchi mbalimbali barani Afrika.

**FAIDA ZA USHIRIKIANO CHINA NA AFRIKA**

Rais Xi anasema mapinduzi ya kuleta maendeleo ni haki ya kila nchi duniani kote na hayazuiliki. Hata hivyo, anasema mchakato wa mapinduzi ya viwanda na maendeleo ya usasa (modernization) katika nchi za Magharibi yamesababisha mateso mengi kwa nchi nyingi zinazoendelea.

Anasema baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, nchi za Dunia ya Tatu, ikiwemo China na Afrika, zilipata uhuru na maendeleo moja baada ya nyingine, na kuanza kurekebisha dhuluma zilizotokana na ukoloni ambapo China hivi karibuni itaadhimisha miaka 75 ya uhuru huo.

Ni katika muktadha huo, Rais Xi anasema Afrika na China zinapaswa kuendelea kushirikiana katika mambo mengi ili kujiletea maendeleo.

Anasema pande hizi mbili zinapaswa kushirikiana kuendeleza na kuimarisha haki na usawa na kwamba katika hilo si kufuata kibubusa sheria



za jumla za maendeleo bali pia kuzingatia hali halisi ya nchi zetu.

"China iko tayari kubadilishana uzoefu wa masuala ya utawala na Afrika, kusaidia nchi kuchunguza njia za kuleta maendeleo zinazolingana na hali zao, na kuhakikisha kunakuwa na haki sawa na fursa sawa kwa nchi zote," anasema.

Anasema China pia iko tayari kuimarisha ushirikiano na Afrika katika kukuza viwanda, kilimo, miundombinu, biashara na uwekezaji.

Katika kukuza raslimali watu Rais Xi anasema: "China iko tayari kushirikiana kwa bidii na Afrika katika mafunzo ya wafanyakazi, kupunguza umaskini na uhaba wa ajira." Pia amesema nchi yake iko tayari kushirikiana na Afrika katika kulinda na kuheshimu imani na tamaduni za kila upande na kushirikiana katika suala zima la uhifadhi wa mazingira. Anagusia kwamba ushirikiano wa China na Afrika si wa kuingilia mambo ya ndani ya nchi hizi huru.

Anasema kuwa maendeleo hayawezi kuja bila kuwepo kwa amani, China iko tayari kushirikiana na Afrika katika suala zima la kulinda amani na utulivu.

"Ni zama mpya za ushirikiano na usasa kati ya China na Afrika, ushirikiano na urafiki wetu uliodumu katika miongo mingi na kuleta aina mpya ya ubia na ushirikiano katika jumuiya ya mataifa sasa tumefanikiwa kufika katika hatua ya juu ya ushikiano wa kimkakati. Nawahakikishia ninyi wote ndugu na marafiki zangu tuliokusanyika hapa kuwa hakuna Taifa lolote litakalosalia nyuma katika safari hii ya usasa (modernization)," anasema.

Mbali na hayo, Rais Xi Jinping ametaja hatua kadhaa zinazotarajiwa kuchukuliwa na serikali yake katika kipindi cha miaka mitatu ijayo (2025-2027) katika kufikia adhima yake ya kusaidia kuleta mageuzi ya maendeleo na usasa barani Afrika ikiwemo utekelezaji wa miradi 30 ya nishati safi, miradi 30 ya mawasiliano, programu 500 za kilimo cha kisasa na kutoa fursa 60,000 za mafunzo hasa kwa vijana na wanawake.

## CHINA NA AFRIKA NI KAKA NA DADA

Rais wa China, Xi anasema urafiki kati ya China na Afrika unavuka mipaka ya muda na umbali, ukipita milima, bahari na mabonde na kwamba umekuwa ni wa kurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Anasema kuanzishwa kwa jukwaa hilo la ushirikiano mwaka 2000 ni hatua muhimu katika historia ya uhusiano kati ya China na Afrika.

"Katika kipindi cha miaka 24 iliyopita, hasa tangu enzi mpya, ndugu na dada wa China na Afrika wameendelea kusonga mbele kwa pamoja kwa moyo wa uaminifu kwa ukaribu na nia njema. Tunasimama bega kwa bega, mkono kwa mkono, na tunatetea kwa uthabiti haki na maslahi halali ya kila mmoja wetu katika mabadiliko ya karne duniani.

"Katika wimbi la utandawazi wa kiuchumi, tumekuwa tukijijenga na kujiimarisha. Tumepata matokeo ya maana ambayo yamewanufaisha mamilioni ya watu wa China na Afrika," anasema.

Anakumbusha pia kwamba China imeshirikiana na Afrika katika kukabiliana na majanga makubwa na milipuko ya magonjwa.

"Daima tumeelewana na kuungana mkono, na kuweka mfano wa aina mpya ya uhusiano wa kimataifa," anasema.

## USHIRIKIANO ULIVYO CHINA NA AFRIKA

Ushirikiano wa China na Afrika umekuwa ukikua kwa kasi katika miongo ya hivi karibuni na kuifanya China kuwa mshirika mkuu wa kibiashara na mwekezaji mkubwa katika bara hili. Ushirikiano huu kabla ya mkutano wa huu wa majuzi umekuwa ukijumuisha maeneo kama biashara, miundombinu, uwekezaji, afya, elimu, na teknolojia.

## BIASHARA

China ni mshirika mkubwa wa kibiashara wa Afrika na biashara kati ya pande mbili hizi imekuwa ikiongezeka kwa kasi.

China inanunua malighafi kama mafuta, madini, na mbao kutoka Afrika, huku Afrika ikiagiza bidhaa za viwandani kama mitambo, magari, na bidhaa za umeme kutoka China.

## MIUNDOMBINU

China imewekeza sana katika miradi mikubwa ya miundombinu barani Afrika, ikiwemo ujenzi wa reli, barabara, viwanja vya ndege, na bandari.

Mfano maarufu ni reli ya kisasa kati ya Mombasa na Nairobi nchini Kenya, inayojulikana kama SGR, iliyofadhiliwa na China. China pia ndio ilijenga reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

## MIKOPO NA MISAADA

Serikali ya China imekuwa ikitoa mikopo yenye masharti nafuu na misaada kwa nchi za Afrika kwa ajili ya maendeleo.

Hata hivyo, kumekuwa na mjadala kuhusu mzigo wa madeni ambao baadhi ya nchi za Afrika zinakabiliana nao kutokana na mikopo hii.

## TEKNOLOJIA NA MAWASILIANO

China pia imekuwa mshirika muhimu katika kuendeleza sekta ya teknolojia ya mawasiliano barani Afrika. Makampuni ya China kama Huawei na ZTE yamekuwa yakijenga miundombinu ya simu na mtandao, pamoja na kuleta teknolojia mpya.

## DIPLOMASIA NA SIASA

China imekuwa na uhusiano wa kidiplomasia na nchi nyingi za Afrika, ikishirikiana katika majukwaa ya kimataifa kama Umoja wa Mataifa. Pia, kupitia Jukwaa la Ushirikiano wa China na Afrika (FOCAC), viongozi wa Afrika na China hukutana kujadili mipango ya ushirikiano.

## ELIMU NA UTAFITI

China imekuwa ikitoa ufadhili kwa wanafunzi wa Afrika kusomea nchini China, huku ikishirikiana katika utafiti wa sayansi na teknolojia. Pia imekuwa ikitoa mafunzo kwa wataalamu wa sekta mbalimbali kutoka Afrika.

Kwa ujumla, ushirikiano wa China na Afrika umeleta faida kwa pande zote mbili, lakini pia kuna changamoto, ikiwemo hofu ya baadhi ya nchi za Afrika kutegemea sana uwekezaji wa China na hasa unaosababisha madeni makubwa.

## UCHUMI WA CHINA

China ni ya pili kiuchumi duniani baada ya Marekani. Inajulikana kwa kuwa na uchumi mkubwa sana kutokana na ukuaji wa haraka katika miongo michache iliyopita.

Pato la Taifa (GDP) la China linafikia takriban dola trilioni 17.7 (kwa takwimu za 2023), ikiwa ni zaidi ya asilimia 17 ya uchumi wa dunia. China imejikita katika uzalishaji wa bidhaa nyingi, biashara ya kimataifa, na uvumbuzi wa teknolojia, na hilo limechangia sana nguvu zake za kiuchumi.

## IDADI YA WATU CHINA

Idadi ya watu nchini China ni takriban bilioni 1.4 (kwa takwimu za 2023). China imekuwa na idadi kubwa zaidi ya watu duniani kwa muda mrefu, ingawa India inatarajiwa kupita China hivi karibuni au tayari imefanya hivyo kulingana na makadirio mengine.

Serikali ya China pia imekuwa ikidhibiti ukuaji wa idadi ya watu kupitia sera kama ile ya "mtoto mmoja," ambayo ilipunguzwa hivi karibuni ili kuruhusu familia kuwa na watoto wawili au zaidi kutokana na changamoto za idadi ya watu kuzeeka.



# Tanzania na China ni pete na chanda

**Na Hamid Yassin**

MUUNGANO wa Tanganyika na Zanzibar ndio chanzo cha ushirikiano wa Kidiplomasia na Jamhuri ya Watu wa China chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Shekhe Abeid Amani Karume kwa kushirikiana na kiongozi aliyeletaapinduzi makubwa China, Mwenyekiti Mao Ze Dong (Mao Tse-Tung) na Waziri Mkuu wake, Zhou Enlai (Chou en Lai) ambao sasa unatimiza miaka 60.

Alama ya Tanzania kwa Taifa la Watu wa China ilisimikwa na Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliposhauri na kupigania Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (The People Republic of China) kujiunga na Umoja wa Mataifa (UN).

Tanzania iliyopambana na Marekani mwaka 1973 kwenye Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa wakati aliyekuwa Rais wa nchi ya Marekani, George Bush Senior alipokuwa Balozi wa Marekani Umoja wa Mataifa na Dk. Salim Ahmed Salim ambaye alikuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa.

Mwana Diplomasia huyo aliwezesha nchi ya China kuchukua kiti chake halali cha Umoja wa Mataifa ambacho kilikaliwa visivyo halali na Taiwan, Taifa ambalo lilikuwa jimbo lililoasi la China kutoka Chama cha Kikomunisti cha China na kujiita Kuomitang chini ya Kibaraka Kai Shekh kuanzia 1947.

Wakati wa Kampeni hizo ujumbe wa Tanzania ukiongozwa na Chifu Patrick Kunambi ulihakikisha China inaingizwa UN na kuigaragaza Marekani ambayo ilianza kununua kura za wajumbe kwa kutoa rushwa wazi wazi kwa hela ambazo Bush alisema anatoa papo kwa papo.

Njama hizo hazikufua dafu kwa diplomasia ya Tanzania, mwishowe China iliingia UN kwa kishindo.

Tanzania ikiwa na mtaji wa nchi zisizofungamana na upande wowote (Non Aligned Countries) zilishinda kwa umoja na lll wao kwani Baraza Kuu kura za turufu (Veto) hazitumiki.

Hii ilikuwa faraja sana kwa China ambayo ilianza kukata tamaa wakati ule wa vita baridi ambapo bpamoja kuwa mwanachama mwanzilishi aliwekewa vikwazo na Marekani kwa kuwa aliunga mkono Taiwan.

Nyakati hizo historia inatuambia siasa za ulimwengu zilikuwa makundi mawili ya Magharibi ikiongozwa na Marekani na Mashariki ikiongozwa na Urusi na hivyo kuanzisha uhasama ambao Marekani ilikuja kulipiza kisasi kwa kura ya Veto mara mbili pale Balozi Dk. Salim Ahmed alipowania Ukatibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na kukataliwa na Marekani.

Wakati wa kuiingiza China UN, Marekani kwa kutumba kwake akaanzisha na kuzusha msemo wa 'banana republics' wa George Bush akiamaanisha nchi ndogondogo zenye uchumi dhaifu ambapo kwa kauli kamili ilikuwa; "The United States cannot be humiliated by the banana republics that it can buy its votes."

Lakini ikashindwa vibaya pamoja na kumwaga fedha nyingi kwani siku zote palipo na ukweli uongo hujitenga; na ukweli siku zote hushinda.



Kwa kuzingatia hayo China na Tanzania ni marafiki wa damu hivyo hufaana kwa dhiki na faraja.

Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere mwana falsafa na mbobezi katika masuala mbalimbali duniani ikiwemo historia alitambua mapema kasoro iliyokuwa pool ya Taifa la Watu wa China kuwakilishwa katika Umoja wa Mataifa na Taifa dogo la kisiwa cha Taiwan.

Hii ilitokana na Jamhuri ya Watu wa China (Bara) kuwa na jumla ya watu milioni 800 wakati na kisiwa cha Taiwan ambacho kilikuwa kinawakilisha China katika Umoja wa Mataifa kikiwa na jumla ya watu milioni 18 tu.

Kutokana na Muungano wetu kuwa na watu mahiri na wana Diplomasia wabobezi, Mwalimu Nyerere alimwagiza Balozi wetu wakati huo katika Umoja wa Mataifa, Dk. Salim Ahmed Salim kuwa ahakikishe China inaingia Umoja wa Mataifa na kuwa mwanachama wa umoja huo, historia hii iliandikwa mwanzoni mwa miaka ya 1970.

Dkt. Salim Ahmed Salim alitoa pendekezo hilo kwenye Umoja wa Mataifa na kuwauliza kwa nini Taiwan ikiwa na idadi ndogo ya watu inaiwakilisha China Mainland kwenye Umoja wa Mataifa badala ya China Mainland kuiwakilisha Taiwan yenye idadi ndogo ya watu na eneo dogo la kijiografia.

Umoja wa Mataifa ukachukua hatua stahiki kwa kukaa kikao na kujadili mapendekezo hayo ya Serikali ya Tanzania juu ya Jamhuri ya Watu wa China kuwa miongoni mwa nchi wawakilishi katika umoja huo na takribani nchi 33 zilipiga kura ili kumpata mwakilishi halali kati ya China mainland na kisiwa cha Taiwan, matokeo yake China (Bara) ilishinda hapo ndipo ilipoanza kujulikana Kimataifa.

Viongozi na wananchi wa mataifa haya ya Tanzania na China wanatambua kuwa, undugu wetu ni wa damu na ni wa muda mrefu. Miaka 60 ya mahusiano mazuri kwa mataifa kutoka mabara tafauti, si suala la mchezo!

Kwa Tanzania nchi ya China ni wenzetu na historia inajieleza ambapo katika miaka ya 1960 nchi nyingi za Bara la Afrika zilikuwa katika vuguvugu la kutafuta uhuru, Tanzania ikiwa miongoni mwao.

Wakati huo China ilikuwa katika vita baridi na Marekani na kiuchumi ilikuwa ni nchi masikini.

Hata hivyo, hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na rais wa kwanza wa Zambia, Kenneth Kaunda walikwenda nchi za magharibi kusema kwamba wanahitaji reli kati ya Tanzania na Zambia kwa sababu reli zilizokuwepo Afrika ya Kusini, Zimbabwe na Msumbiji zilikuwa zikiendeshwa kwa ubaguzi. Nchi za magharibi hazikukubali ombi hilo.

Lakini walipokwenda China kuomba msaada huo wa ujenzi, ingawa China wakati huo haikuwa miongoni mwa nchi zilizoendelea ilijibu kwamba reli hiyo itajengwa kwa ushirikiano.

Wachina wakashiriki katika ukombozi wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambapo walijenga Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ambayo mpaka leo inajulikana kama Reli ya Uhuru.

Mwenyekiti Mao Ze Dong na Waziri Mkuu Chou en Lai wa China walikuwa marafiki wa Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa la Tanzania na urafiki huo umedumishwa hadi leo.

China imeimarika na kuwa mshirika mkubwa wa Afrika kiuchumi. Fedha zinazotoka China kuelekea Afrika zimekuwa zikiongezeka tofauti na zamani.

China imekuwa ikitoa misaada na kuwa mfadhili mkuu wa fedha katika kutekeleza miradi mingi ya miundombinu ambayo inashuhudiwa Barani Afrika na Tanzania kwa ujumla katika miaka ya hivi karibuni. Hakuna nchi inayoweza kulingana na kiwango chake cha ushirika.

Kutokana na hali hii, biashara imeinuka wa asilimia 20 kila mwaka, katika kipindi cha mwongo mmoja na nusu uliopita. Zipo kampuni zaidi 10,000 za China zinazofanya kazi barani Afrika hiyo ikiwa ni mara nne zaidi ya makadirio ya awali.

Inakadiriwa kuwa asilimia 90 ya kampuni hizo ni zile za binafsi katika sekta tofauti huku theluthi moja zikijikita katika viwanda.

Kampuni hizo zinachangia kwa mitaji ya uwekezaji, maendeleo ya usimamizi na ujasiriamali katika sekta mbalimbali Barani Afrika. Kwa kufanya hivyo, zinasaidia kukuza maendeleo ya uchumi wa nchi za Afrika. Tunaamini kuna nafasi ya kuendelea zaidi.

Mbali na viwanda, robo ya kampuni za China zimejikita katika utoaji huduma kwenye biashara na ujenzi. Tayari asilimia 12 za mapato ya viwanda vya Afrika hutokana na kampuni za China, hiyo ikikadiriwa kuwa ni jumla ya dola bilioni 500 kwa mwaka.

Kwa upande wa miundombinu, China imechukua asilimia 50 ya soko la Afrika kuhusu uhandisi, ununuzi na ujenzi. Kampuni za China zinapata faida nzuri na kurejesha fedha zao za mtaji kwa muda wa mwaka mmoja au chini ya muda huo.

Kampuni hizo zinalenga zaidi matakwa ya masoko ya Afrika yanayokua kwa kasi kuliko kulenga kwenye bidhaa za kuuza au kusafirisha nje ya Afrika. Uwekezaji wao unaashiria ushirikiano wa kudumu kwa Afrika. Kampuni za China zina matumaini ya mustakabali mzuri wa Afrika.

Uwekezaji na biashara Barani Afrika unaofanywa na China unaleta faida kuu za kiuchumi kama vile kubuni nafasi za ajira na taaluma, kubadilishana ujuzi na teknolojia na pia ni ufadhili na maendeleo ya miundo mbinu.

Imani na alama aliyoiweka Mwalimu Nyerere na shujaa wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Sheikh Karume pamoja na Muungano, ndio inayotufanya tutembee kifua mbele na kuthaminiwa kwa kiasi kikubwa na Jamhuri ya Watu wa China.

Ambapo wakati sisi tarehe 26 Aprili mwaka huu 2024 tulisherekea kumbukizi ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, wao wanaadhimisha siku ya kumbukumbu ya Ushirikiano wa Kidiplomasia wa Tanzania na China kutimiza miaka 60!

Hii ziara ya Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan alizozifanya hivi karibuni China zinachangia katika kuendeleza uhusiano na undugu wa mataifa haya ulioanzishwa na waasisi wa mataifa haya, Mwalimu Nyerere, Abeid Karume, Mao Ze Dong na Waziri Mkuu wake, Chou en Lai.

Ziara hiyo ya kikazi nchini China kuanzia Septemba 2 hadi 6, 2024 imemwezesha Rais Dk. Samia kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (Forum on China-Africa Cooperation-FOCAC) jijini Beijing, China.

*Kwa maoni na ushauri;*
*0768 888 787 ama 0784 122 020.*




# Tazara itakavyonufaika na ziara ya Dk. Samia China

**Na Hamid Yassin**

SEPTEMBA 5 wiki iliyopita, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alihutubia Mkutano wa Tisa wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) uliofanyika Beijing China. Katika hotuba yake, alisisitiza umuhimu wa kufufua Reli ya Tanzania na Zambia (Tazara), ambapo China imeahidi kuunga mkono hatua hiyo kwa kiasi kikubwa.

Makubaliano hayo, yaliyosainiwa mbele ya Rais Xi Jinping wa China na Rais Hakainde Hichilema wa Zambia, yanalenga kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kuimarisha biashara za kikanda.

Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza nafasi ya Tanzania kama kitovu cha kikanda kwa ajiri ya biashara na usafirishaji.

Aidha, wakati wa ziara hiyo Rais Dkt. Samia alikutana na mwenyeji wake, Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China kwa mazungumzo yanayolenga kuimarisha uhusiano mzuri na wa kihistoria kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China ulioasisiwa miaka 60 iliyopita.

Pamoja na mambo mengine, miongoni mwa maeneo yanayotarajiwa kupewa kipaumbele kwenye Mkutano wa FOCAC ni uendelezaji wa miundombinu, kukuza uwekezaji, uendelezaji wa viwanda, kilimo cha kisasa na amani na usalama.

Rais Dk. Samia alikuwa miongoni mwa wakuu wa nchi waliohutubia ufunguzi wa Mkutano wa FOCAC akizungumza kwa niaba ya Kanda ya Afrika Mashariki.

Pia katika ziara hii, Rais Dk. Samia amekutana na makampuni na wawekezaji kutoka Jamhuri ya Watu wa China kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji zaidi nchini Tanzania.

Rais Samia pia alibainisha umuhimu wa ushirikiano katika sekta ya kilimo, biashara na teknolojia rafiki wa mazingira. Katika hotuba hiyo, aliunga mkono mipango ya China kuwekeza dola bilioni 50 barani Afrika kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo, kwa lengo la kuimarisha miundombinu, kukuza biashara, na kuunda ajira mpya

### KUBORESHA RELI YA TAZARA

Katika ziara hii ya China, Dk. Samia alizungumza na kukubaliana na mwenyeji wake, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Xi Jinping, kuboresha Reli ya Tazara akiwa sambamba na Rais wa Zambia, Mhe. Hakainde Hichilema.

Uboreshaji huu wa reli ya Tazara siyo tu utayaongezea mataifa haya mawili, Tanzania na Zambia nafasi za ajira, bali utaboresha ustawi wa jamii na kuinua viwango vya kiuchumi kwa nchi hizi.

Haya yote ni kutokana na nchi ya China mbali ya kukubali kuboresha Reli ye Tazara, pia imeahidi kuendelea kuwekeza katika miradi ya kimkakati ya Tanzania ikiwemo miundombinu ya kidigitali na usimamizi wa rasilimali za bahari. Hii ni dhahiri kuwa ziara ya Rais Dk. Samia nchini China itakuwa na athari chanya katika uchumi wa Tanzania.

### UHUSIANO WA TANZANIA, ZAMBIA NA CHINA

Kama ilivyo Tanzania na China, hata jirani zetu Zambia uhusiano wetu ni wa siku nyingi ambao uliimarishwa na viongozi waasisi wa mataifa haya, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na hayati, Kenneth Kaunda.

### VINARA WA UKOMBOZI

Kihistoria Tanzania na Zambia zimeshiriki kwa pamoja kuongoza harakati na mapambano ya ukombozi Kusini mwa Afrika huku Tanzania ikiwa ndio Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi. Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere tangu TANU na ASP hadi CCM yake na Kenneth Kaunda na UNIP yake walifanya kazi kubwa sana ya kudai uhuru wa Kusini mwa Afrika.

Makambi mengi ya Wapigania uhuru wa Msumbiji, Zimbabwe, Afrika Kusini, Namibia, Angola na Botswana yalikua kwenye nchi hizi mbili, hivyo Zambia ni wenzetu kihistoria kwa hiyo jambo lao lolote ni letu na ni muhimu kuendeleza umoja huu mkubwa kati yetu na wao.

### USHIRIKIANO WA KIUCHUMI

Zambia ni 'Landlocked State', yaani hawana bahari; hivyo bidhaa zao nyingi wanategemea kuingiza na kutoa nchini mwao kupitia Bandari yetu ya Dar es Salaam, Tanzania.

Haishangazi kabisa kwa Rais Dk. Samia kushirikiana na Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema katika kusaini ule mkataba wa kuboresha reli ya Tazara, kwani ukitoa nchi ya Kenya, Zambia ni washirika wakubwa wa pili kiuchumi pamoja na Congo DRC hapa kwetu.

Hili halishangazi hata kidogo kuona nchi yetu ikiwa mstari wa mbele na masuala ya Zambia sababu yana maana kubwa katika uchumi wetu.

Takwimu za mwaka 2023, Tanzania ilisafirisha bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 92.7 kwenda Zambia nyingi zikiwa bidhaa za ujenzi na vifaa mbalimbali vya mashine huku Zambia ikisafirisha bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 71.4 hasa bidhaa za kilimo na madini ya shaba.

### USHIRIKIANO WA MIRADI YA KIMKAKATI

Mwaka 1968 nchi hizi mbili zilishirikiana kujenga Bomba la Mafuta (TAZAMA) lenye urefu wa Km 1710 kutoka Dar es Salaam Tanzania hadi Ndola Zambia ambalo husafirisha tani milioni 1.1 za mafuta kwa mwaka.

Bomba hili la TAZAMA linamilikiwa kwa pamoja na nchi hizi mbili kupitia kampuni ya TAZAMA PIPELINE LTD ambapo Zambia wana asilimia 66. na Tanzania asilimia 33.3 ya umiliki. Hivyo ushiriki wetu Zambia kwenye masuala yao mbalimbali una faida kubwa sana kwetu wa kuendelea kuimarisha miradi hii mikubwa ya kimkakati na kuendelea kujenga uchumi wetu vyema.

### USHIRIKIANO WA KIDIPLOMASIA

Nchi hizi mbili zina uhusiano wa kihistoria wa kidiplomasia huku Zambia ikiwa na Ofisi za Ubalozi jijini Dar es Salaam sanjari na Tanzania inayo Ofisi za Ubalozi Lusaka nchini Zambia.

Pia hata kwenye suala la utalii wa nchi hizi mbili raia wake hawahitaji visa kutembelea vivutio vya utalii.

Februari Mwaka 2015, Rais wa Tanzania wa wakati huo, Jakaya Kikwete alifanya ziara rasmi ya Kiserikali ya siku mbili nchini Zambia na Novemba 26, 2019 Rais Edgar Lungu alifanya Ziara nchini Tanzania na alifanya mazungumzo rasmi na Rais wa awamu ya tano, hayati John Pombe Magufuli.

### USHIRIKIANO WA KIMIUNDOMBINU

Ujenzi wa reli ya TAZARA kuanzia mwaka 1970 hadi 1975 kwa msaada wa nchi ya China ni ushahidi tosha kwamba nchi hizi mbili ni zaidi ya majirani. Reli ya Tazara (Tanzania-Zambia Railway) yenye urefu wa KM 1860, ililenga kusafirisha madini ya shaba kutoka Zambia kuleta Bandari ya Dar es Salaam. Reli hii ya TAZARA hadi hii leo ipo na bado inafanya vizuri ikisimamiwa na nchi zote mbili.

### HITIMISHO

Jumanne Agosti 24 mwaka 2021, aliapishwa Rais mpya wa Zambia Hakainde Hichilema wa Chama Cha UPND (United Party for National Development) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia alikuwa ni miongoni mwa Marais waliohudhuria sherehe hizo za kuapishwa kwake.

Msafara wa Rais Samia uliwabeba viongozi wa Serikali na CCM ukiongozwa na ndugu Shaka Hamdu Shaka ambaye wakati huo alikuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Itikadi na Uenezi, Mjumbe wa Kamati kuu na Waziri Mkuu Mstaafu wa Serikali ya awamu ya 4 Mhe. Mizengo Peter Pinda.

Walikuwepo pia viongozi wengine wa Chama na Serikali kwenye msafara huo; Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete alikuwepo pia Lusaka nchini Zambia tangu mwanzo wa uchaguzi kama Kiongozi wa jopo la Waangalizi wa uchaguzi huo kutoka Jumuiya ya Madola.

Kwa nini Rais aliongozana na viongozi wa Chama na Serikali kwenye safari ya Zambia ya uapisho ule wa Haikainde?

Ifahamike kwamba uhusiano wa Tanzania na Zambia ni tunu na inapaswa kuendelea kulindwa kama anavyofanya Rais Dk. Samia.

Hii inatukumbusha kihistoria na kwa kiasi kikubwa Tanzania ndio wanufaika wakubwa wa ushirikiano huu hivyo kitendo cha Dk. Samia kuongozana na viongozi wa Chama na Serikali hakukosea bali amejikita katika kuendelea kulinda mahusiano baina ya Zambia na Tanzania.

Zambia imepata Rais mpya tena kutoka Chama Cha Upinzani hivyo vyovyote vile msafara wake pamoja na kwenda kuimarisha uhusiano wa kiuchumi, kidiplomasia na kindugu, lakini ametumia nafasi hiyo hiyo kuanzisha mahusiano mahususi kati ya Chama Cha Mapinduzi na Chama kipya tawala cha Zambia cha UPND (United Party for National Development) ili uhusiano wetu mkubwa na Zambia usitetereke hata baada ya kuingia kwa uongozi mpya.

Ni dhahiri kama Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Tanzania pamoja na wasaidizi wake ndani ya Chama na Serikali wamechanga vizuri karata hii ikiwa ni dhahiri sasa uhusiano huu wenye faida lukuki za kiuchumi kwetu utaendelea kuimarika na kuboreka zaidi.

Kama ilivyofanyika juzi kule nchini China kwa viongozi wetu hawa kusaini mkataba wa kuboresha reli ya Tazara mbele ya rafiki yetu mwingine mkubwa, Rais wa China, Xi Jinping ambaye amebariki nchi yake kusaidia uboreshaji huo.

*Kwa maoni na ushauri;*
*0768 888 787 ama 0784 122 020.*



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# CCM inavyokataa wagombea wa kusafisha na dodoki

MBUNGE wa Chalinze (CCM) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, amewahi kutoa ushauri maridhawa kwa viongozi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa makini katika kuwapata viongozi bora hasa kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Katika ushauri wake, Ridhiwani amesema: "Hata kama kuna mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi ambaye yeye mwenyewe mnamwona wala hataki mambo hayo, jamii pale inamtaja vizuri, mfuateni na mumwambie kama wewe mwenzetu kila tukikaa kijiweni, tunasema kama kuna mtu mzuri wa kutuongoza basi ni yule pale ambaye ni wewe utatuletea mambo mazuri eneo letu. Basi mfuateni na mwambie ili kukisaidia Chama chetu. Lakini kutafuta wale marafiki zenu ambao mnauza nao mapori, kutafuta marafiki zenu mnaofanya nao ubadhirifu wa mali za umma, ni kukiingiza Chama kwenye mtihani mkubwa sana."

Nimeanza makala haya kwa kukumbushia nukuu hii muhimu ambayo kama ikizingatiwa vyema, basi CCM itakuwa na kazi rahisi ya kupata ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na ule uchaguzi mkuu wa mwakani.

Ridhiwani amewaasa viongozi na wanachama kuhakikisha hawafanyi makosa muda wa kupitisha wagombea wa kupeperusha bendera ya CCM kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuhakikisha wanawapitisha wagombea bora ikibidi hata kumshawishi mwanachama wa CCM ambaye hataki kugombea, lakini ni chaguo la wananchi, ajitokeze kugombea ili kuipa CCM ushindi.

Wananchi shida yao ni kupata viongozi bora wenye moyo wa utumishi ndani yao ili kuwatumikia na kuhakikisha kero zao zinatatuliwa kujenga ustawi bora wa maisha yao ya kizazi cha sasa na kijacho.

Katika kuelekea kwenye chaguzi hizi mbili, timu za kampeni huundwa na vyama vya siasa ili kuratibu zoezi zima la kunadi ilani, sera na wagombea wa vyama vyao ili kupata uungwaji mkono wa wananchi na hatimaye chama kushinda kwa kishindo kwenye chaguzi na kupata ridhaa ya kuongozi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Nimefuatilia kauli za viongozi



mbalimbali wa CCM pamoja na walezi wa CCM katika mikoa mbalimbali nchini, wote kwa kauli moja wamedhamiria kuhakikisha kuwa katika chaguzi hizi, Chama kinasimamisha wagombea bora hasa wanaokubaliwa na wananchi ili kurahisisha ushindi katika chaguzi.

Uzoefu unaonyesha kuwa mgombea bora, mzalendo, mchapakazi na anayekubalika kwa wananchi ana nafasi kubwa ya kuchaguliwa na wananchi na kushinda bila kufanya mikutano mingi ya hadhara ya kuomba ridhaa ya kuwatumikia wananchi katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Akihutubia mkutano wa hadhara kwenye uwanja wa Furahisha Jijini Mwanza Agosti 15, 2024, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, CPA Amos Makalla aliwahakikishia wananchi kuwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa na ule mkuu wa mwakani,

CCM itawapelekea wagombea wenye sifa, wasio na makandokando wenye malengo ya kuwaletea maendeleo.

"Niseme nisiseme, Niseme nisisemee? Mimi ndiye Katibu

> **Hatutaleta mgombea ambaye kesi zote za viwanja anahusika yeye, hatutaleta wagombea wa kusafisha na dodoki, tutaleta wagombea walio safi. Tunataka kushinda kwa ushindi wa heshima wa asilimia 99.9.**

Mwenezi wa CCM, nataka niwahakikishie CCM itawaletea wagombea safi, wasio na makandokando ambao wako tayari kuwaletea wananchi maendeleo. Mko tayari?, mko tayari?" amesema Makalla.

Mkazo huu uliowekwa na Mwenezi Makalla ni muhimu kuzingatiwa, hii itasaidia sana kabla ya mtu kuamua kuchukua fomu ya kugombea nafasi fulani ya uongozi ajipime mwenyewe kama anafaa kuwa kiongozi au ili asiwe sababu ya kuifanya timu ya kampeni kuanza kumsafisha kwa tuhuma mbalimbali zinazomkabili badala ya kutumia muda vyema kumnadi mgombea na sera za Chama ambazo zimelenga kutatua kero za wananchi na kuwaletea maendeleo.

Vilevile, Mwenezi Makalla ambaye pia ni Mlezi wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, akiwa Kigamboni kwenye mkutano wa hadhara amesema "Hatutaleta mgombea ambaye kesi zote za viwanja anahusika yeye, hatutaleta wagombea wa kusafisha na dodoki, tutaleta wagombea walio safi. Tunataka kushinda kwa ushindi wa heshima wa asilimia 99.9."

Ni muhimu kwa wote wenye mpango wa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi hasa ndani ya CCM, kujipima kuona kama kweli hawana makandokando ambayo yatasababisha kuenguliwa kwao katika kinyang'anyiro cha uchaguzi.

Hakuna haja ya kupitisha jina la mgombea ambaye anapaswa kusafishwa na dodoki wakati wapo wanachama wengi wazuri, wenye weledi na moyo wa kuwatumikia wananchi ambao kupitia hao, ushindi utakuwa ni kama kumsukuma mlevi kwenye sanduku la kura. Katika kupigilia msumari wa moto kusisitiza kuwa CCM haitapitisha wagombea wenye makandokando, CPA Makalla amesema "Wasiosoma taarifa za mapato na matumizi ya vijiji, uchaguzi ujao hawana nafasi. Jitahidini mchague wenyeviti ambao hawana makandokando, hatutaki mgombea ambaye tumwoshe kwa dodoki na sabuni. Tunataka mtu ambaye tukimpeleka kwa wananchi, wanamkubali na hakuna minong'ono. Chagueni watu sahihi ambao watatoa matumaini kwa CCM. Chama kinataka uchaguzi wa kishindo na heshima."

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Maeneo makuu ya uwekezaji wa maana kwenye maisha



KAMA tulivyoona wiki iliyopita, yapo maeneo ambayo watu walio na ufahamu, busara na nguvu ya akili wanayapa kipaumbele kuwekeza kwayo. Wiki iliyopita, tuliangazia kwa undani maeneo matatu makuu na vipengele vyake. Mambo hayo ni:

(1) Uwekezaji kwa Mungu, (2) Uwekezaji kwenye Afya

(3) Uwekezaji kwenye Maarifa.

Kutokujua vipaumbele hivi vya uwekezaji wako au kuyaacha mambo hayo, ndiyo hunasababisha maisha yetu kukosa mwelekeo. Tafadhali ungana nami tuendelee sehemu ya pili tuone vipaumbele vingine vya uwekezaji wenye maana kama ifuatavyo: -

4. Uwekezaji wa kiuchumi

Ni mchakato wa kutumia rasilimali, kama vile fedha, muda na juhudi, kwa ajili ya kupata faida ya kifedha au kuboresha hali ya kiuchumi katika siku zijazo.

Uwekezaji huu unaweza kufanyika kwa njia mbalimbali na unalenga kuimarisha mtaji, kuongeza mali au kuleta mapato kwa muda mrefu.

Zifuatazo ni baadhi ya aina na dhana kuu zinazohusiana na uwekezaji wa kiuchumi:

Aina za Uwekezaji wa kiuchumi

A. Uwekezaji wa moja kwa moja (Direct Investment):

B. Uwekezaji wa kifedha (Financial Investment):

C. Uwekezaji wa raslimali (Capital Investment):

D. Uwekezaji wa kimataifa (Foreign Investment):

Malengo ya Uwekezaji wa kiuchumi

A. Kupata faida:

B. Kuongeza utajiri:

C. Kupunguza hatari (Diversification): Kuwekeza katika aina tofauti za mali na masoko, husaidia kupunguza hatari kwa kuweka fedha zako katika maeneo tofauti.

D. Kukuza uchumi: Uwekezaji unachangia ukuaji wa uchumi kwa kuongeza uzalishaji, ajira na maendeleo ya miundombinu.

Kwa ujumla, uwekezaji wa kiuchumi unalenga kutengeneza thamani kwa wawekezaji na kuchangia katika ukuaji wa uchumi kwa ujumla. 5. Uwekezaji kwa watu

Hapa kuna aina mbili za uwekezaji huu. Aina ya kwanza ni kutumia rasilimali, muda, na juhudi ili kuboresha maisha, ujuzi na uwezo wa watu binafsi au jamii kwa ujumla. Lengo la uwekezaji huu ni kuendeleza vipaji, kuongeza ustawi wa watu na kusaidia watu kufikia uwezo wao kamili, ambayo kwa upande wake, inachangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Lakini leo naizungumzia aina ya pili ya uwekezaji kwa watu ambayo ni mchakato wa kujitolea kuboresha uhusiano wako na watu wengine, kukuza ustadi wa kijamii na kujenga sifa ya kuwa mtu anayejali, anayehusiana vizuri na wengine na mwenye uwezo wa kushirikiana na wengine kwa ufanisi. Hii inahusisha kujitahidi kuwa na mahusiano mazuri, kusaidia wengine na kujenga mtandao wa kijamii ambao ni wenye msaada na unawiana.

Hapa kuna baadhi ya njia za kujiweka kuwa mtu wa watu:

A. Kujenga ujuzi wa mawasiliano
- Kusikiliza kwa makini:
- Kujieleza kwa ufanisi:

B. Kuwa na huruma na uelewa
- Kuelewa hisia za wengine:
- Kujali na kutoa msaada:

C. Kujenga mitandao ya kijamii
- Kujihusisha na watu.
- Kushirikiana

D. Kujenga sifa nzuri
- Uaminifu na uadilifu:
- Kujali maadili na heshima:

E. Kuonyesha uvumilivu na ustahimilivu
- Kuvumilia changamoto za mahusiano:
- Kujifunza kutoka kwa makosa:


F. Kuendeleza ustadi wa uongozi wa kijamii
- Kuwa mshauri na kiongozi:
- Kushiriki ujuzi na maarifa:


Kujiwekeza kuwa mtu wa watu ni juhudi ya kujijenga kuwa mtu anayeaminika, anayependa kushirikiana na anayejali maslahi ya wengine. Mtu wa watu huthaminiwa kwa mchango wake wa kijamii na uwezo wake wa kujenga uhusiano wenye maana na wa kudumu.

Kama ungependa kupata ushauri au usimamizi wa karibu katika kuishi mwongozo huu, (Unaweza kuwa taasisi, kikundi, kanisa, umoja, NGO au mtu binafsi), karibu sana tutashirikiana nawe kwa neema na msaada wa Mungu. Karibu uwasiliane nasi kwa namba 0676055444 au barua pepe mngongopaul@yahoo.com

We work Consult
Your Partner in Growth.

# Utata wa kifo cha JF Kennedy wa Marekani-2






**Wiki iliyopita tulianza simulizi hii ya utata wa John Fitzgerald Kennedy, alikuwa Rais wa 35 wa Marekani na kuhudumu kuanzia Januari 20, 1961 mwaka 1961 hadi alipouawa Novemba 22 mwaka 1963. Ikiwa ni ni miaka 61 imepita tangu kifo hicho, wiki iliyopita tuliangalia safari yake ya kutembelea Jimo la Texas akiwa na malengo kadhaa, kubwa likiwa ni kujiimarisha kisiasa katika jimbo hilo baada ya kutofanya vizuri sana katika uchaguzi uliokuwa umemwingiza madarakani. Mwandishi Wetu, HAMID YASSIN anaendelea kutiririka na mkasa mzima wa mauaji yale kwa msaada wa mashirika ya habari ya kimataifa.**

Safari ya Kennedy kutembelea Texas ilitangazwa rasmi kwa umma mwezi Septemba mwaka 1963.

Mpangilio wa ruti ambayo msafara wake ungepita ulikamilika kupangiliwa tarehe 18 Novemba na kutangazwa asubuhi ya Novemba 22 ili wananchi wajitokeze barabarani kumlaki.

Taarifa ya Ikulu ambayo iliwasilishwa kwa 'Secret Services' ilionesha kwamba ndege ya Rais ingeruka kutoka Kiwanja cha Ndege wa Kijeshi wa Carswell Airforce Base maeneo ya Fort Worth na kwenda kutua uwanja wa Dallas Love Field.

Baada ya hapo Rais Kennedy alikuwa anatakiwa kusafiri kwa msafara wa gari kutoka Kiwanja cha Dallas Love Field na kuelekea eneo la Dallas Trade Mart ambako Kennedy alitarajiwa kupata chakula cha mchana na wenyeji wake.

Ruti hii ilipangwa na kupendekezwa na rafiki mkubwa wa Kennedy aliyeitwa Kenneth O'Donnell ambaye alikuwa pia ndiye katibu wake aliyehusika na masuala ya teuzi za watumishi wa ngazi za juu serikalini.

Ruti hii iliyokuwa inapendekezwa kutoka Kiwanja cha Ndege cha Dallas Love Field mpaka Dallas Trade Mart ambayo ilikuwa na urefu wa kilomita 16 na ilikuwa inategemewa kuchukua takribani dakika 45 kwa mwendo wa taratibu ili kumpa nafasi Kennedy kuwasabahi wananchi kwa kuwapungia mkono.

Ratiba hii pamoja na ruti iliyopendekezwa iliwasilishwa ofisi ya 'Secret Services' ambapo maafisa waliohusika nayo kuipokea na kuiwekea mkakati wa kiusalama walikuwa ni 'Special Agent', Winston G. Lawson ambaye alikuwa ni 'advance Secret Services agent' (afisa ambaye yuko kwenye Whitehouse Detail kwa ajili ya kumlinda Rais moja kwa moja). Pia alikuwa pamoja Agent Forrest V. Sorrels ambaye huyu ni 'Special Agent' ambaye anahusika na ofisi ya 'Secret Services' eneo la Dallas.

Maafisa usalama hawa wawili walikutana mara kadhaa kuweka mkakati wa kiulinzi kwa ajili ya safari hii ya Rais ya Novemba 22.

Moja ya vikao vyao hivyo walikifanya tarehe 14 Novemba kwenye uwanja wa ndege wa Dallas Love Field ambapo baada ya kikao waliendesha gari pamoja kupita njia ile ambayo imependekezwa msafara wa Rais uje kupita wiki moja baadaye.

Siku hii ya tarehe 14, maafisa hawa walipokuwa wanaendesha gari kupita kwenye hii ruti inayopendekezwa kuna jambo waliliona, jambo ambalo liliwashitua kidogo na kuwafanya waingie wasiwasi juu ya hii ruti inayopendekezwa. Endapo jambo hili lingezingatiwa, basi Kennedy asingeuwawa wiki moja baadaye!

Swali kwa nini waliingiwa na wasiwasi baada ya kuona hicho walichokiona lakini bado msafara wa Kennedy ukapita ruti hii hii wiki moja baadaye? Au swali la msingi zaidi waliona kitu gani?

## DALLAS

Msafara wa Rais ulipokamata barabara kuingia katikati ya mji wa Dallas kuelekea Trade Mart ulikuwa kwenye mpangilio ufuatao;

## GARI YA MBELE

Gari ya mbele kabisa iliyokuwa inaongoza msafara ilikuwa ni gari aina ya Frord Mercury Sedan. Aliyekuwa anaendesha gari hii alikuwa ni Mkuu wa Idara ya Polisi katika mji wa Dallas ambaye aliitwa, Jesse Curry.

Katika siti ya mbele ya mkono wa kulia alikuwa ameketi Afisa wa Secret Services , Special Agent (Jasusi ukipenda) Winston.

Siti ya nyuma ya gari hii mkono wa kushoto alikuwa ameketi Bill Decker, Sheriff wa mji wa Dallas na siti ya mkono wake wa kulia alikuwa ameketi afisa mwingine wa Secret Services, SAIC, Forrest Sorrels (SAIC - Special Agent In Charge).

## GARI YA RAIS

Gari hii ambayo Rais Kennedy alipanda ilikuwa ni aina ya Lincoln Continental Convertible ya mwaka 1961, ambayo iliboreshwa ili kukidhi masuala ya kiusalama na iliendeshwa na afisa wa Secret Services Agent, William Greer. Pembeni yake katika siti ya mbele alikuwa ameketi afisa mwingine wa Secret Services, ASAIC Roy Kellerman (ASAIC - Assistant Special Agent In Charge).

Huyu ndiyo yule afisa ambaye alipewa maagizo na O'Donnel swahiba wa Kennedy na katibu wake anayeshughulika na masuala ya Teuzi, kuwa kama hakutakuwa na mvua mjini Dallas basi ahakikishe kuwa gari atakayopanda Rais inakuwa wazi bila paa la juu ili kuwarahisishia wananchi kumwona Rais wao kwa uzuri na kupungiana mikono.

Viti vya nyuma (za katikati) mkono wa kulia alikuwa amekaa Gavana Connally huku mkono wake wa kushoto akiwa amekaa mkewe, Nellie Connally.

Viti vya nyuma kabisa vya gari hii ya wazi, mkono wa kulia alikuwa ameketi Rais Kennedy huku mkono wake wa kushoto akiwa ameketi mkewe Jacqueline Kennedy.

Pembezoni ubavuni mwa gari ambalo alikuwa amepanda Rais Kennedy, kulikuwa na pikipiki mbili za polisi kila upande, ambapo mkono wa kushoto kulikuwa na pikipiki zilizoendeshwa na polisi wa kituo cha mji wa Dallas, ofisa, Billy Joe Martin na ofisa, Bobby Hargis.

Upande wa kulia kulikuwa na pikipiki zilizoendeshwa na ofisa James M. Cheney na ofisa Douglas L. Jackson.

## GARI YA NYUMA YA RAIS (FOLLOW UP CAR)

Nyuma ya gari aliyopanda Rais Kennedy kulikuwa na gari aina ya Cadillac Touring Convertible ambayo iliwabeba maafisa wa Secret Services kwa ajili ya ulinzi wa Rais na na mkewe (First Lady).

Dereva wa gari hili alikuwa ni Agent Sana Kinney. Pembeni yake siti ya mbele kulia aliketi ATSAIC Emory Roberts (Assistant To Special Agent In Charge).

Katika mlango wa mbele mkono wa kushoto, kwenye mlango alikuwa ananing'inia Special Agent Clint Hill, ambaye anahusika na ulinzi wa First Lady.

Kwenye mlango mwingine wa mbele kulia alikuwa ananing'inia Special Agent Jack Ready.

Mlango wa nyuma kulia alikuwa ananing'inia Special Agent Paul Landis huku mlango wa mkono wa kushoto alikuwa ananing'inia Special Agent, William T. McIntyre.

Ndani ya gari siti ya nyuma walikuwa wameketi watu wanne. Kulikuwa na Kenneth O'Donnell msaidi wa rais na katibu wake wa masuala ya teuzi, pia kulikuwa na David Powers ambaye naye ni msaidizi wa Rais na pambeni yao hawa mkono wa kulia aliketi Special Agent Glen Bennet na mkono wa kushoto aliketi Agent George Hickey.

*Itaendelea*

# Mafuriko yaua watu 341 Chad



**N'DJAMENA, Chad**

WATU 341 wamefariki dunia na wengine milioni 1.5 kuathirika kufuatia mafuriko makubwa ya wiki kadhaa nchini Chad Julai, mwaka huu Umoja wa Mataifa (UN) umesema.

Ofisi ya UN ya Kuratibu Misaada ya Kibinadamu (OCHA), ilisema majimbo 23 ya nchi hiyo yalikumbwa na mafuriko hayo.

Ilitaja takwimu za serikali ambazo zilisema baadhi ya nyumba 164,000 zimeharibiwa, karibu ng'ombe 70,000 walikufa na ekari 640,000 za mashamba pia ziliharibiwa.

Serikali bado haijatangaza takwimu rasmi za uharibifu huo uliosababishwa na mafuriko ambayo yamekumba taifa hilo lenye watu milioni 16.

Wiki iliyopita, wanafunzi 14 na mwalimu wao, walifariki dunia basi lao lilipoanguka baada ya mvua kubwa kunyesha katika Jimbo la Ouaddai eneo la Mashariki lenye ukame.

Kufikia katikati ya Agosti, mwaka huu, watu 54 walipoteza maisha kutokana na mafuriko katika Jimbo la Tibesti, kwenye jangwa la Chad eneo la mbali la Kaskazini.

# ...yaua wengine 18 Morocco



**RABAT, Morocco**

WATU 18, wakiwemo raia wa kigeni, wamefariki dunia na wengine wanne kutoweka kutokana na mafuriko Kusini mwa Morocco.

Wizara ya Mambo ya Ndani ilisema juzi ikisahihisha idadi ya awali ya watu 11 waliotangazwa kupoteza maisha yao.

10 kati yao walifa dunia katika Mkoa wa Tata na watatu huko Errachidia, akiwemo raia wa Canada na mwingine wa Peru, wizara hiyo ilisema.

Iliongeza kuwa watu wengine wawili walipoteza maisha huko Tiznit, wawili huko Tinghir, akiwemo raia wa Uhispania na mwingine alifariki huko Taraoudant.

Hata hivyo, Wizara haikufafanua ikiwa raia hao wa kigeni walikuwa wakazi au wageni.

Tangu Ijumaa iliyopita, maeneo yenye ukame Kusini mwa Morocco, yamezama katika mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa, maafisa walisema. VOA.

## Blinken ziarani Uingereza kujadili mzozo wa Ukraine

**WASHINGTON, Marekani**

WAZIRI wa Mambo ya Kigeni wa Marekani, Antony Blinken, amewasili Uingereza kwa ziara itakayojumuisha mazungumzo mapana na serikali ya nchi hiyo ambayo yanatarajiwa kugusia vita vya Ukraine na mzozo wa Mashariki ya Kati.

Akiwa jijini London, Blinkenanatarajiwa kukutana na Waziri Mkuu wa Uingereza, Kier Starmer na Waziri mwezake wa Mambo ya Nchi za Nje, Matthew Miller.

Ziara yake inafanyika siku kadhaa kabla ya Starmer kuitembelea Marekani kwa mazungumzo na Rais Joe Biden jijini Washington.

Kiongozi huyo atasafiri siku ya Ijumaa kwenda Marekani kwa mkutano na Rais Biden ambao utakuwa wa pili tangu chama chake cha Labour kiliposhinda uchaguzi Julai, mwaka huu.

Marekani na Uingereza zinashirikiana kwenye masuala yote makubwa ya kimataifa na Starmer ameweka wazi azma yake ya kuendelea kuimarisha nafasi ya Uingereza ya kuiunga mkono Ukraine katika vita vyake dhidi ya Urusi.

Serikali yake pia imechukua msimamo madhubuti dhidi ya Israel ikiishinikiza kufanya inaloweza kupunguza madhila ya wakazi wa Ukanda wa Gaza.

Serikali ya Starmer pia imezuia baadhi ya mauzo ya silaha kwa Israel ikisema ina wasiwasi zinaweza kutumika kukiuka sheria za kimataifa. VOA.



# Mashambulizi ya Israel yaua watu 40 Gaza

**GAZA, Palestina**

TAKRIBAN watu 40 wameuawa Kusini mwa Gaza na makumi ya wengine kujeruhiwa katika mashambulizi ya Israel kwenye eneo lililochaguliwa kuwa la kibinadamu, Mamlaka ya Ulinzi wa Raia inayosimamiwa na Hamas, imesema.

Jeshi la Israel limesema ndege yake ilishambulia kitovu cha operesheni zilizofanywa na Khan Younis eneo la wapiganaji wa Hamas na kwamba imechukua hatua za kupunguza hatari ya kuwadhuru raia.

Wakazi wa eneo hilo walisema mashambulizi matatu yalilenga mahema ya watu waliokimbia makazi yao katika eneo la kibinadamu la al-Mawasi, Magharibi mwa Jiji la Khan Younis na kusababisha mashimo makubwa.

"Watu 40 waliuawa na zaidi ya 60 kujeruhiwa, huku wengi wakiwa bado chini ya vifusi," Mkurugenzi wa Operesheni wa Mamlaka ya Ulinzi wa Raia wa Hamas aliambia BBC.

Walioshuhudia waliambia BBC milipuko mikubwa ilitikisa eneo la al-Mawasi muda mfupi baada ya saa 6:00 usiku na miali ya moto ilionekana kupanda angani.

Khaled Mahmoud, mfanyakazi wa kujitolea wa shirika la kutoa misaada ambaye anaishi karibu na eneo la lililoshambuliwa, alisema yeye na watu wengine waliojitolea, walikimbilia kusaidia, lakini walishangazwa na ukubwa wa maafa.



"Mashambulizi hayo yalisababisha mashimo matatu yenye kina cha mita saba na kufukia mahema zaidi ya 20," Mahmoud alisema.

Video ambazo hazijathibitishwa, zilionesha raia wakichimba mchanga huo kwa mikono wakijaribu kuwaokoa Wapalestina kutoka kwenye shimo refu lililosababishwa na mashambulizi hayo ya anga.

Akiweka ujumbe kwenye mtandao wa Telegram, Msemaji wa Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) alisema limewashambulia "magaidi muhimu wa kundi la Hamas ambao walikuwa wakisimamia shughuli zao kwa kutoa amri na kudhibiti eneo lililotengwa kuwa la kibinadamu huko Khan Younis." BBC.

# Tamasha Faraja ya Tasnia ni mfano wa kuigwa



**Na Hamid Yassin**

## ● Dk. Samia azikabidhi familia za wafiwa mkono wa pole



TAASISI ya Mama Ongea na Mwanao chini ya uongozi wa Steven Mengere almaarufu kama 'Steve Nyerere' hauna budi kupongezwa kwa kuandaa Tamasha kubwa la 'Faraja ya Tasnia' la kuwaenzi wasanii wenzao na wadau wengine wa tasnia hiyo waliotangulia mbele ya haki.

Nimeelezwa kuwa, Tamasha hili lipo muda sasa, lakini lilikuwa linafanyika kimyakimya kwa kushirikisha watu wachache bila ya kuwa na hadhi kama hii tuliyoiona Septemba 7 pale Viwanja vya Leaders.

Mbali ya lengo kuu la kuwarehemu wasanii wote walitangulia mbele ya haki, lakini kupitia Tamasha hili la Faraja ya Tasnia mambo mengi yaliyo nyuma ya pazia yanayowasibu wasanii walio hai na familia za marehemu yamejulikana.

Wasanii, wadau wa sanaa na viongozi wa kada mbalimbali wakiwemo wale wa dini, walipata fursa ya kueleza kila kilicho mioyoni mwao na nini kifanyike kuanzia sasa ili kuzikabili changamoto zao wakiwa kazini na baada ya kustaafu ama kutangulia mbele ya haki.

Nisingependa kuwa mwongeaji mkuu katika hili, bali nawachia wasanii na wadau mbalimbali waliofunguka mengi kupitia Tamasha hilo la Faraja ya Tasnia hapa chini.

Mchekeshaji na mwigizaji mkongwe nchini Tanzania, Lucas Lazaro maarufu Joti amesema kuwa, amefarijika na kufurahi baada ya kuona picha ya aliyekuwa mwigizaji Alhaji Amri Athumani maarufu Mzee Majuto katika tamasha la Faraja ya Tasnia.

"Kwa kuona picha ya mmoja kati ya wasanii nguli baba yangu (Mzee Majuto), nimefarijika sana lakini pia nimefarijika kuwaona baadhi ya wasanii wengine ambao nimewahi kufanya nao kazi, uzuri King Majuto nishafanya naye kazi, halikadhalika akina Mama Abduli, Kanumba, Korongo na wengine wengi kwa hiyo mimi najisikia faraja sana na hii itaweka historia kubwa sana katika tasnia yetu," amesema Joti

Aidha, Joti ameongeza kuwa, anaamini kuwa tamasha hilo litaweka historia kubwa katika tasnia hiyo.

Naye Mwigizaji Irene Uwoya amesema licha ya kuingia kwenye maisha ya wokovu hawezi kufuta tatoo zilizopo mwilini mwake hadi roho mtakatifu atakapomwambia.

Uwoya ameyasema hayo Septemba 7, 2024 wakati akizungumza katika tamasha hilo la Faraja ya Tasnia lililofanyika katika viwanja vya Leaders Club jijini Dar es salaam.

"Sisi binadamu tunaishi mambo ni mengi hapa duniani unapoamua kujikataa na kumfuata Mungu siyo jambo dogo linachukua muda hata mimi kuna muda nashindwa naona kama nakata tamaa lakini maombi ndiyo silaha," amesema.

Wakati Uwoya akitumia fursa ya tamasha hilo kutangaza ulokole wake, muigizaji mkongwe nchini Tanzania, Ahmed Olotu, maarufu kama Mzee Chillo, amesema kuwa pengo la Kanumba ndiyo pekee ambalo mpaka sasa halijazibika huku akiongeza kuwa kwenye upande wa uigizaji, kuna vijana wengi wanaojitahidi na kufanya vizuri.

Mama wa marehemu Steven Kanumba, Flora Mtegoa amesema anamkumbuka sana mwanawe kwa vingi ikiwemo upendo wake, utashi na vingine vingi huku akisema alikuwa kila kitu kwake.

Flora ambaye naye hivi sasa amejitosa kwenye uigizaji, amesema tangu mwanaye afariki dunia hajawahi kuangalia filamu yake hata moja kwa sababu zinamuumiza licha ya kuwa anazikubali kazi hizo.

"Kwanza tangu ameondoka duniani siangaliagi movie (filamu) yake hata moja. Kwa hiyo movies zote mimi nazipenda ila siangaliagi nimejitahidi sana lakini hilo limenishinda," amesema Mama Kanumba.

Kanumba alizaliwa Januari 8, 1984 mkoani Shinyanga na alifariki dunia Aprili 7, 2012 akiwa na umri wa miaka 28.

Marehemu Kanumba alitamba na filamu kama 'Magic House', 'Big Daddy', 'This is it', 'Kijiji cha tambua haki' na nyinginezo nyingi.

Mbali na hayo mama wa mwigizaji Othman Njaidi 'Patrick Kanumba' amesema Kanumba amejenga historia kubwa kwenye maisha ya kijana wake.

"Kanumba ana historia kubwa sana kwenye maisha ya Patrick kuliko hata kaka zake aliozaliwa nao, kwa sababu Kanumba ndiyo alikuwa amemshika mkono amemtoa kwenye fani hii na kila kukicha anamkumbuka, hajawahi kumsahau hata siku moja," amesema mama mzazi wa Patrick aliyeingizwa kwenye maigizo na marehemu Kanumba.

Mama Patrick aliendelea kueleza kuwa, kuna mipango ambayo mwanaye ameiandaa kwa ajili ya kumuenzi Kanumba pamoja na kusherehekea kutimiza miaka 15 katika tasnia ya uigizaji.

Utakumbuka kuwa Kanumba ndiye alivumbua kipaji cha Patrick alifanikiwa kuigiza naye filamu kama "Uncle JJ" "This is it" na nyinginezo.

Aliyekuwa mgeni rasmi kwenye Tamasha hilo, Mshauri wa Rais kwenye masuala ya Sanaa, Angellah Mbelwa Kairuki amesema kuwa, Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za wasanii lakini pia kufanyia kazi changamoto wanazozipitia.

Pia Kairuki alikabidhi zawadi maalum toka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa familia za wasanii waliotangulia mbele ya haki.

Naye Katibu wa Baraza la Sanaa la Taifa (Basata), Kedmond Mapana amewapongeza wasanii kwa kuandaa tamasha la Faraja ya Tasnia kwani wameonyesha heshima kubwa kuwakumbuka wasanii wenzao ambao ni marehemu.







# Ifahamu historia ya mpira wa wavu Tanzania

## ● TVF waleta nuru kwenye mchezo huo



**Na Valensi Mbaga**

WAKATI mchezo wa mpira wa wavu nchini Tanzania ukikua kwa kasi hivi sasa, baadhi ya mabadiliko yamekuwa chanya sana na jitihada zote hizo zimefanywa na Shirikisho la mpira wa wavu Tanzania (TVF) zamani TAVA ambapo mpaka sasa nuru ya mchezo huo inaonekana wazi.

Tanzania ikiwa ni moja kati ya nchi yenye nguvu katika mchezo huo na inazalisha wachezaji bora duniani kote na kushinda medali katika mashindano ya kimataifa.

Wavu 'Volleyball' ilikuja Tanzania kwa mara ya kwanza mwanzoni mwa miaka ya 1920, wakati wakoloni wa Uingereza, walowezi wa Kizungu, na wamisionari walipouleta miaka hiyo.

Ushahidi wa mchezo huu unaweza kupatikana nyuma kama 1911, wakati timu mbili za Askari wa Uingereza zilikuwa na mechi dhidi ya kila mmoja hapa nchini.

Muda si muda ikawa burudani ya kupendwa, na kulikuwa na vilabu vingi jijini Dar es Salaam kabla ya miaka ya 1930. Leo, bado ni maarufu miongoni mwa Watanzania na mara nyingi hufurahia ufukweni.

Timu mbili za wanajeshi wa Uingereza zilicheza mechi ya kwanza rasmi ya mpira wa wavu nchini Tanzania mwaka wa 1922, lakini hadi 1955 ndipo shirikisho la kwanza la mpira wa wavu lilianzishwa.

Shirikisho la kwanza la kitaifa la mpira wa wavu lilianzishwa mnamo 1954, na chini ya shirikisho hilo timu iliyoanzishwa ilifanya mazoezi yake na kujiandaa na michuano ya kimataifa kwenye Mashindano ya Afrika ya 1956, na kumaliza katika nafasi ya nne.

Tangu wakati huo, Tanzania imekuwa ikishiriki mara kwa mara katika mashindano makubwa kama vile Michezo ya Afrika na Kombe la Mataifa ya Afrika.

Kipindi cha kukumbukwa zaidi kwa mpira wa wavu wa Tanzania ni katika Michezo ya Olimpiki ya mwaka 1980 mjini Moscow wakati timu ya taifa ilipoushangaza ulimwengu kwa kuishinda China katika robo fainali.

Katika miaka ya hivi karibuni, mpira wa wavu umekua maarufu nchini Tanzania miongoni mwa watu wa kila rika na uwezo.

Timu ya Taifa ya Tanzania ya mpira wa wavu imejinyakulia tuzo nyingi za kimataifa na kujivunia baadhi ya wachezaji bora wa mpira wa wavu duniani.

Mchezo huu umekuwa muhimu katika kuunganisha watu kutoka asili tofauti, kukuza fahari ya kitaifa, na kuwapa vijana ujuzi na kujiamini.

Zaidi ya yote, imeunda utamaduni unaojumuisha zaidi ambapo kila mtu anaweza kushindana kwa misingi ya kawaida.

Baada ya miaka kupita sasa mchezo wa mpira wavu Tanzania ukageuka na kuwa na sura mpya. Haukuishia kuwa mchezo wa kujifurahisha tu, bali ajira kwa Watanzania walio wengi na maboresho mbalimbali katika nyenzo tofauti za mchezo huo zikafanyika.

Yote hayo yalifanyika kikamilifu chini ya usimamizi wa Shirikisho jipya la mchezo huo TVF ambalo limeendesha Ligi Kuu ya mchezo huo kwa kukutanisha vilabu kutoka katika kona mbalimbali za nchi ya Tanzania kujumuika na kutoa burudani kwa wananchi kupitia mchezo huo.

Japokuwa kuna mafanikio mengi lakini bado zipo changamoto nyingi zinazozuia maendeleo chanya ya mchezo huo na hivyo kwa pamoja wadau mbalimbali na sekta binafsi zinapaswa kuunga mkono jitihada za Shirikisho la mchezo wa mpira wa wavu ili kuinua zaidi mchezo huo.



# Kutana na wanasoka nyota wanaosota sokoni












**LONDON, England**

DIRISHA la usajili la majira ya kiangazi limefungwa na vilabu vya Ligi Kuu England vimetumia mamilioni ya pauni kuimarisha vikosi vyao.

Lakini timu ambazo zilikosa kutimiza malengo yao, bado zina nafasi ya kuwaleta wachezaji huru, wachezaji ambao hawana mkataba na wanaweza kusaini klabu yoyote.

Hapa kwenye makala haya tunakuletea baadhi ya wachezaji ambao bado wako sokoni.

### KIPA - KEYLOR NAVAS

Keylor Navas, 37, alitangaza kuondoka Paris St-Germain mwezi Mei na aliripotiwa kujiunga na Monza ya Italia kwa uhamisho wa bure wakati mkataba ulipoisha.

Kipa huyo wa zamani wa Costa Rica alitumia miaka mitano Real Madrid na mingine mitano PSG. Pia alicheza mechi 17 za Ligi Kuu England wakati wa mkopo huko Nottingham Forest msimu wa 2022-23.

### BEKI WA KULIA - SERGE AURIER

Beki wa zamani wa Tottenham na Nottingham Forest Serge Aurier, 31, alicheza pamoja na nyota wa zamani wa Crystal Palace, Wilfried Zaha huko Galatasaray mwishoni mwa msimu uliopita kabla ya kuondoka msimu wa joto.

Beki huyo wa Ivory Coast mwenye uzoefu mkubwa ni mshindi mara mbili wa Ligue 1 akiwa na Paris St-Germain.

### BEKI WA KATI - JOEL MATIP

Joel Matip, 33, aliiaga Liverpool msimu wa joto baada ya misimu minane.

Aliisaidia klabu hiyo kushinda Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya chini ya Jurgen Klopp baada ya kujiunga na Liver akitokea Schalke kwa uhamisho wa bure.

Matip tangu wakati huo amekuwa akihusishwa na vilabu kadhaa ikiwemo West Ham.

### BEKI WA KATI - MATS HUMMELS

Mshindi wa Kombe la Dunia la 2014 nchini Ujerumani, Mats Hummels aliichezea Borussia Dortmund fainali ya Ligi ya Mabingwa mwezi Juni waliposhindwa na Real Madrid kwenye Uwanja wa Wembley.

Ilikuwa ni mechi ya mwisho ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 katika klabu hiyo. Hummels, ambaye ameichezea pia Bayern Munich, amekuwa akihusishwa kuhamia Roma.

### BEKI WA KUSHOTO - BRANDON WILLIAMS

Brandon Williams, 24, alikuwa na umri wa miaka 19 alipoifungia Manchester United katika sare ya 3-3 katika Ligi Kuu England dhidi ya Sheffield United mwaka 2019.

Williams, alikuwa na United tangu akiwa umri wa miaka tisa, aliachiliwa msimu wa joto baada ya mechi 51 za kikosi cha kwanza.

Kwa sasa yupo huru na hana klabu mpya.

### WINGA - VICTOR MOSES

Victor Moses, 33, anatafuta klabu mpya baada ya kuondoka Spartak Moscow.

Moses alicheza mechi 220 za Ligi Kuu England kwa vilabu vitano, vikiwemo Chelsea na Liverpool.

Alikaa Chelsea kwa miaka tisa kati ya 2012 na 2021 baada ya kujiunga kutoka Wigan kwa pauni milioni 9.

### KIUNGO WA KATI - ADRIEN RABIOT

Adrien Rabiot, 29, aliondoka Juventus mwishoni mwa kandarasi yake akiwa amecheza mechi 212 na timu hiyo ya Serie A baada ya kusajiliwa kutoka Paris St-Germain mwaka 2019.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chuo cha Michezo cha Manchester City, amekuwa akihusishwa na Manchester United. Rabiot aliichezea Ufaransa katika fainali ya Kombe la Dunia 2022 walipopoteza kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Argentina.

### KIUNGO WA KATI - ANDRE GOMES

Andre Gomes, 31, aliondoka Everton, ambayo ilimnunua kwa pauni milioni 22 mwaka 2019, na mkataba wake umeisha baada ya msimu wa 2023-24.

Wasifu wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno unajumuisha kuichezea Barcelona, Valencia na Lille.

Ripoti zinasema Gomes huenda akahamia Marekani kucheza MLS lakini bado hana klabu.

### MSHAMBULIAJI - ROBERT SKOV

Robert Skov, 28, aliwahi kuelezwa kuwa ni mbadala wa Gareth Bale kwa Denmark. Mshambuliaji huyo anahusishwa na Tottenham. Alicheza Kombe la Dunia 2022 lakini anabaki bila klabu baada ya miaka mitano nchini Ujerumani akiwa na Hoffenheim.

Skov alicheza zaidi ya mechi 100 za Bundesliga, akifunga mara 11.

### MSHAMBULIAJI - ANTHONY MARTIAL

Manchester United ilitangaza mwezi Mei, kuwa Anthony Martial ataondoka klabuni hapo baada ya kufunga mabao 90 katika mechi 317 alizocheza.

Mshambulizi huyo wa Ufaransa ana umri wa miaka 28 na bado hana klabu.

Ripoti nchini Ufaransa, zinasema Lille, ambayo itamenyana na Liverpool katika Ligi ya Mabingwa msimu huu, inavutiwa na Martial na wanashughulikia dili la kuinasa saini yake.

### MSHAMBULIAJI - MEMPHIS DEPAY

Memphis Depay, 30, aliisaidia Uholanzi kufika nusu fainali ya Euro 2024.

Anawindwa na klabu mpya baada ya kukosa nafasi msimu 2023/24 akiwa na Atletico Madrid, kwa sababu ya jeraha.

Mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United alikaa kwa miezi 18 Barcelona na pia amewahi kucheza Ufaransa katika klabu ya Lyon.

# Kona ya Urembo



# Urembo na mwonekano mzuri wa midomo

Na Hidaya Machupa

MIDOMO ni moja ya sehemu muhimu sana za uso zinazovutia, na kwa miaka mingi zimekuwa zikizingatiwa sana katika mitindo na urembo. Kuwa na midomo inayovutia huongeza mvuto wa sura kwa ujumla.






**Midomo ni sehemu muhimu ya uso, inayochangia uzuri na mvuto wa mtu. Urembo wa midomo huanzia na afya yake, na hii inahitaji uangalizi maalum kutokana na sifa za kipekee za ngozi ya midomo. Daktari wa ngozi anaweza kutoa ushauri mzuri juu ya jinsi ya kudumisha afya na urembo wa midomo.**

### MBINU ZA KUBORESHA UREMBO WA MIDOMO

Midomo ni miyembamba na haina tezi za mafuta, hivyo huwa rahisi kukauka.

### KUZUIA MIDOMO KUKAUKA NA KUPASUKA:

Tumia 'Lip Balm', Weka 'lip balm' yenye unyevunyevu mara kwa mara, hasa kabla ya kulala na unapokuwa nje kwenye hali ya hewa ya baridi au ya jua kali.

Dr. Joshua Zeichner, wa ngozi wa New York, anasema kuwa kujichubua 'exfoliation' midomo ni muhimu kwa kuondoa seli zilizokufa na kusaidia midomo kuwa laini.

Hata hivyo, anaonya kuwa kujichubua inapaswa kufanywa kwa uangalifu ili kuepuka kuikwaruza midomo na kusababisha uharibifu.

### EPUKA KULAMBA MIDOMO

Kulamba midomo kunaondoa unyevunyevu wa asili, na kufanya midomo yako kuwa kavu zaidi. Maji ni muhimu sana kwa afya ya ngozi, ikiwemo midomo.

Kuondoa ngozi iliyokufa kama ilivyo kwenye ngozi nyingine, midomo yako pia inahitaji kuichubua ili kuondoa ngozi iliyokufa na kuifanya iwe laini.

Unaweza kutumia dawa 'scrub' maalum ya midomo mara 2-3 kwa wiki. Dawa hizi za kusugua huondoa seli za ngozi zilizokufa na kuacha midomo ikiwa laini na angavu.

Unaweza kutengeneza dawa 'scrub' ya asili nyumbani kwa kutumia sukari na mafuta ya nazi. Sukari inasaidia kujichubua, wakati mafuta ya nazi yanachangia katika kulainisha na kulainisha midomo.

### KUJIPAMBA MIDOMO KUNONGEZA MVUTO WA USO

Chagua rangi za 'lipstick' zinazokufaa kulingana na rangi ya ngozi yako. Rangi nyekundu na 'nude lipstick' ni maarufu sana na zinaweza kuvaliwa kwa hafla mbalimbali.

Kwa wale wanaopenda mng'ao wa asili, 'lip gloss' ni chaguo bora. Inaongeza unyevu na kufanya midomo ionekane yenye afya.

Zana ya 'Lip liner' inasaidia kuipa midomo mwonekano wa umbo zuri na kuzuia 'lipstick' isichuruzike. Tumia 'lip liner' yenye rangi inayofanana na 'lipstick' yako kwa matokeo bora.

### MIDOMO INAWEZA KUATHIRIKA NA MIONZI YA JUA

Afya ya jumla ya midomo ni pamoja na lishe bora, Chakula chenye vitamini C na E kinasaidia kuimarisha afya ya ngozi na midomo. Hakikisha unakula matunda na mboga kwa wingi.

Uvutaji wa sigara unaweza kuharibu midomo na kusababisha midomo kuwa na mistari ya mapema.

### AFYA YA MIDOMO

Midomo ni sehemu muhimu ya uso, inayochangia uzuri na mvuto wa mtu. Urembo wa midomo huanzia na afya yake, na hii inahitaji uangalizi maalum kutokana na sifa za kipekee za ngozi ya midomo. Daktari wa ngozi anaweza kutoa ushauri mzuri juu ya jinsi ya kudumisha afya na urembo wa midomo.

Afya ya midomo inahitaji utunzaji wa hali ya juu na kwa kufuata ushauri wa madaktari wa ngozi, unaweza kuhakikisha kuwa midomo yako inabaki na afya, laini, na yenye mvuto.

Urembo wa midomo unaanza na utunzaji wa afya yake, na kuongeza vipodozi vya ubora husaidia kuboresha mwonekano wake zaidi.

Midomo ni sehemu muhimu ya uso na inaweza kuboresha mwonekano wako kwa kiasi kikubwa. Kwa kufuata hatua zilizotajwa, unaweza kuwa na midomo yenye afya, inayovutia, na inayoakisi uzuri wako wa asili. Kumbuka kwamba urembo wa midomo huanza na utunzaji wa afya ya midomo, na kisha unaweza kuongeza urembo zaidi kwa kutumia vipodozi mbalimbali.







Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Septemba 11-17, 2024 |

# Gidabuday afariki dunia



Na Mwandishi Wetu

ALIYEWAHI kuwa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Wilhelm Gidabuday amefariki dunia.

Inaelezwa Gidabuday amefariki dunia saa 7 usiku wa kuamkia jana Jumanne Septemba 10, 2024 baada ya kugongwa na gari eneo la Maji ya Chai, mkoani Arusha.

Mjumbe wa Riadha Kanda ya Mashariki, Alfredo Shahanga amethibitisha kuwa, kiongozi huyo amefariki baada ya kugongwa kwenye eneo hilo akiwa ameshuka kwenye gari akielekea nyumbani kwake.

"Ni kweli Gidabuday hatunaye," amesema Shahanga kwa masikitiko.

Shahanga anasema kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hili, Gidabuday alipoteza maisha hapo hapo baada ya kugongwa.

# Simba yaifuata Al Ahly kibabe

Na Mwandishi Wetu

KIKOSI kamili cha wawakilishi wa Tanzania kwenye Michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba kimeondoka leo alfajiri kuelekea Tripoli nchini Libya tayari kwa mechi yao ya Septemba 15 dhidi ya wenyeji wao, Al Ahly Tripoli.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadlu Davids ametamba kuwa, wanakwenda Libya wakiwa na matumaini makubwa ya kufanya vema kwani sasa kikosi chake kipo barabara kwa michuano hiyo ya Afrika.

"Najua nao wamesajili nyota wapya kadhaa na wana kikosi kizuri hivi sasa, lakini nimeiandaa timu yangu vema na nina imani kubwa tunakwenda kupata ushindi," aliongea kocha huyo.

Kocha huyo raia wa Afrika Kusini amepasha kuwa, sasa amekamilisha rasmi mafunzo ya mwanzo wa msimu (pre season) kama taratibu za soka zinavyotaka huku akitamba kwamba vijana wake wamepokea vizuri mafundisho yake.

"Sasa kikosi changu kimeiva barabara, yamebakia masuala machache ya kiufundi kwa sababu kuna wachezaji walichelewa kujiunga na kambi, tunakwenda Libya kuikabili Al Ahly Tripoli tukiwa vema, wajiandae kwa upinzani mgumu toka kwetu," amejinasibu Fadlu.

Juu ya wachezaji wao walioko kwenye timu zao za taifa, Fadlu amepasha kuwa, mipango imeshafanywa na viongozi ili wachezaji hao wajiunge na wenzao Libya moja kwa moja wakitokea kwenye timu zao za taifa.

Katika hatua nyingine kocha Fadlu amenena kuwa, kiungo mshambuliaji wa Simba anayeongoza kwa asisti kwa sasa katika Ligi Kuu Bara, Jean Charles Ahoua yuko fiti kwa asilimia 100 tayari kuivaa Al Ahli Tripoli baada ya kuwa nje kwa majeraha na kumpa furaha Kocha wake huyo.

Ahoua alibainika kupata majeraha madogo ya misuli mara baada ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Fountain Gate na alifunga bao moja wakati Simba ikishinda 4-0 na kuanzishiwa programu maalumu na kocha wa viungo, Riedoh Berdien na kumfanya akose mechi ya kirafiki ya sare 1-1 kati ya timu hiyo na Al Hilal ya Sudan.

Nyota huyo mpya aliyesajiliwa msimu huu kutoka timu ya Stella Abijan ya Ivory Coast, alicheza mechi ya pili ya kirafiki ya Simba inayojiandaa kuvaana na Walibya katika Kombe la Shirikisho Afrika, wakati waalipoifunga JKT Tanzania, huku akifunga pia bao moja katika ushindi wa 2-0.




# Taifa Stars yaichapa Guinea kwao

## ● Rais Dk.Samia awaahidi milioni 500 ikifuzu Afcon



Na Mwandishi Wetu

TIMU ya taifa, Taifa Stars imefufua matumaini ya kucheza tena Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika mwakani nchini Morocco baada ya kuichapa Guinea bao 2-1 nyumbani kwao.

Kipindi cha kwanza mpira ulianza kwa timu zote mbili kushambuliana kwa zamu huku Guinea ikifanya hivyo mara nyingi zaidi.

Stars iliyofanyiwa mabadiliko ya wachezaji watatu katika eneo la ushambuliaji kutoka katika kile kikosi kilichoanza dhidi ya Ethiopia, nayo ilichangamka kiasi lakini hakukuwa na umaliziaji mzuri.

Dakika ya 10 tu ya mchezo beki, Dickson Job aliumia jichoni na nafasi yake ikachukuliwa na Bakari Mwamnyeto.

Kipa wa Guinea, Ibrahim Kone aliokoa timu yake kufungwa dakika ya 13 ya mchezo baada ya kupangua vizuri shuti la Waziri Junior.

Guinea nao walijibu mapigo dakika ya 15 kwa shambulizi kali, lakini shuti kali lililopigwa na Ibrahim Diakite lilipanguliwa na kipa, Ally Salimu kuwa kona tasa.

Kipindi cha pili Guinea walikuja na kasi kama ya kimbunga wakisaka goli la kuongoza na wakakosa bao la wazi dakika ya 54, lakini dakika mbili baadae walirekebisha makosa yao na kufunga bao la kuongoza kupitia mshambuliaji wao, Mohamed Bayo.

Bao hilo liliwastua Stars na kuanza kupeleka mashambulizi mfululizo kwenye lango la Guinea na juhudi hizo zilizaa matunda dakika ya 60 baada ya kiungo mshambuliaji, Feisal Salumu kufunga bao la kusawazisha kwa shuti kali la umbali mrefu.

Mpira uliendelea kwa mashambulizi mfululizo hususan Guinea wakilishambulia lango la Stars kama nyuki, lakini walikuwa Taifa Stars waliowaduwaza wenyeji wao kwa bao la kushtukiza la dakika ya 88 kupitia Mudathiri Yahya.

Wakati huo huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan ameahidi kutoa shilingi milioni 500 kama Tanzania itafuzu AFCON 2025.

Naibu Waziri Utamaduni, Sanaa na Michezo Hamis Mwinjuma (Mwana FA) alisema hayo wakati anazungumza na wachezaji wa Taifa Stars muda mfupi kabla ya kuelekea uwanjani kwenye mchezo wa kufuzu AFCON 2025 dhidi ya Guinea.

"Nimepewa salamu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk, Samia kama tutafanikiwa kufuzu AFCON 2025 pale Morocco basi Rais atatoa shilingi milioni mia tano (Tsh Milioni 500)," amepasha Mwinjuma.

# Kocha Azam FC asifu soka la Tanzania

Na Mwandishi Wetu



KOCHA mpya wa Azam FC, Rachid Taoussi amesifu soka la Tanzania na kubainisha kwamba ni nchi ambayo imepiga hatua kubwa kwenye soka la Afrika katika miaka ya hivi karibu.

Rachid amepasha kuwa, unaweza kuthibitisha hilo kwa kuangalia ushiriki wa timu kama Simba kwenye hatua kubwa za Ligi ya Mabingwa Afrika na ile michuano ya African Football League.

Kocha huyo kutoka Morocco ametanabahisha kuwa, mradi mkubwa wa uwekezaji wa Azam FC, ubora na ukubwa wa ligi ya Tanzania ndiyo umechangia yeye kukubali dili la kuja kufanya kazi na 'Wanalambalamba' hao.

# Niang achukua nafasi ya Mzize Wydad




Na Mwandishi Wetu

BAADA ya juhudi za kumnasa mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize kushindikana, klabu ya Wydad Casablanca ya Morocco, imemsainisha mshambuliaji wa zamani wa AC Milan, M'baye Niang, kama mchezaji huru kufuatia kuisha kwa mkataba wake na klabu ya Empoli ya Italia.

Niang mwenye miaka 29, alizichezea klabu kadhaa za Ulaya kama AC Milan ya Italia, Montpellier ya Ufaransa, Watford ya England, Torino ya Italia na Rennes ya Ufaransa.

Wydad ilimfukuzia sana Mzize kiasi cha kuongeza dau mara mbili hadi kufikia dola za Marekani 400,000 ambazo ni sawa na Tsh. 1,087,482,532, lakini klabu yake Yanga 'iliwachunia'.